Gazeti la kwanza la Kiislamu kutolewa kwa lugha ya Kiswahili mwaka 1936.

Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na cho chote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri. (24:56).

لَا إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ

MAPENZI YA MUNGU

TOLEO MAALUM LA KARNE YA UKHALIFA

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 69 NO. 142 JAMADI-UL-AKHIR 1429 AH TOLEO MAALUM LA KARNE YA UKHALIFA (MEI 2008) IHSAN 1387HS BEI SH. 500/=

UKWELI WA MTUME MUHAMMAD S.A.W. WAZIDI KUNG'AA

UKHALIFA

WATIMIZA KARNE MOJA

- ***Ni ule ulioanzishwa na Masihi Wake, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s.)***
- ***Mwenyezi Mungu Athibitisha ukweli wake kwa mashambulizi ya Kimbinguni***
- ***Maadui zake wakata tamaa na kufadhaika***



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu Khilafat Ahmadiyya imetimiza miaka 100. Wanajumuiya wa Jamaat Ahmadiyya nchini wanaungana na Wanajumuiya wenzao duniani kote katika kuadhimisha karne hiyo ya Ukhalifa.

Ukhalifa wa Ahmadiyya umeanzishwa tarehe 27 Mei 1908 baada ya kifo cha Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ambaye ni Masihi Aliyeahidiwa.

Hadhrat Ahmad a.s. alieleza kwamba kwa ajili ya kutimiza ukweli wake, Mwenyezi Mungu ataanzisha nidhamu ya Ukhalifa baada ya kifo chake. Kwa karne nzima sasa, Mwenyezi Mungu ameendelea kuonesha kwamba anaiunga mkono Khilafat Ahmadiyya kama maelezo haya mafupi juu ya historia ya Makhalifa inavyoonyesha:

Endelea uk. 2



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih V a.t.b.a

1. HADHRAT MAULANA HAKEEM NURUDDIN,



Maulana Hakeem Nuruddin Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.



Hadhrat Mirza Bashiruddin Hadhrat Khalifatul Masih II r.a.



Hadhrat Mirza Nasir Ahmad Hadhrat Khalifatul Masih III r.h.a



Hadhrat Mirza Tahir Ahmad Hadhrat Khalifatul Masih IV r.h.a.

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

Mapenzi ya Mungu

MAONI YETU

UKHALIFA NA MAJUKU-MU YETU

Wakati Mwenyezi Mungu Ametujaalia kushuhudia karne moja ya Ukhalifa wa Kiahmadiyya ni jambo la msingi kwetu kukumbuka ubeti wa Kiajemi uliotungwa na Masihi Aliyeahidiwa - Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s) kumhusu sahaba wake mpenzi Hazrat Nurudin. Ubeti huo unasema "Ingekuwa furaha ilioje kama kila mfuasi wangu angelikuwa kama Nurudini".

Maombi na mapenzi ya Masihi Aliyeahidiwa ni kuwa kila Ahmadiyya awe kama Hadhrat Nurudin yule Khalifa tul Masih – I. Je, Alikuwa na sifa gani? Mwana ulamaa huyu alizunguka Dari-madari kwa madhumuni ya kutafuta elimu. Wanajumuiyya tunao wajibu mkubwa wa kutafuta elimu na sio kutafuta elimu tu isipokuwa kuwashinda wengine katika uwanja huo kama alivyoonyesha Profesa Abdus Salaam na Sir Muhammad Zafrullah Khan. Mapenzi ya Hadhrat Nurudin yalikuwa makubwa yaliyotoka kwenye maneno na kufikia kwenye vitendo. Aliacha zahanati yake na akayatoa maisha yake yote kumtumikia Masihi Aliyeahidiwa. Ni lazima kwa maendeleo yetu tuongeze mapenzi yetu kwa Masihi Aliyeahidiwa mwana wa kiroho wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) kama alivyofanya Nurudini. Tuende zaidi ya maneno na tuonyeshe mapenzi hayo kwa vitendo. Inatubidi kutanguliza dini na kujitolea kwa hali na mali ili kuhakikisha ujumbe aliokuja nao Masihi Aliyeahidiwa unafika pembe nne za dunia. Huu ni wito ambao Makhalifa wote wa Masihi Aliyeahidiwa wamekuwa wakiutoa. Na mwaminio siku zote kazi yake ni kusikia na kutii. Wakati tunaadhimisha karne moja ya Ukhalifa wa Kiahmadiyya tukumbuke kuwa Jahazi iliyotuvusha salama katika mawimbi haya ya karne moja ni kusikia na kutii. Msingi mkubwa wa kusikia na kutii ni Taqwa. Na hayo ndiyo yalikuwa maisha ya Hadhrat Nurudin. Inasimuliwa hotuba nzima ya ijumaa alitoa sentensi moja 'Takullah – mcheni Mwenyezi Mungu' na hotuba ikawa imekwisha. Kuwatumikia viumbe wa Mwenyezi Mungu kwa mapenzi na huruma lilikuwa katika damu yake.

Ahmadiyya ni mti uliopandwa na Allah na hakuna nguvu yoyote inayoweza kuung'oa. Tunalotakiwa nasi tutoe mchango wetu ili asaa nasi tukakubaliwe kama walivyokubaliwa wapenzi wa Allah.

KARNE MOJA YA UKHALIFA

Kutoka Uk. 1

KHALIFATUL MASIH I

Hadhrat Maulana Alhaj Hakim Nurudin alikuwa Khalifa wa kwanza wa Masih Aliyeahidiwa a.s. Alizaliwa mwaka 1841 huko Bhera katika jimbo la Punjab India, sehemu ambayo kwa hivi sasa ni sehemu ya taifa la Pakistan. Ukoo wake una mnasaba na Khalifa wa pili wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Hadhart Omar bin Khatab r.a. Ukoo wake toka mwanzo ulikuwa na mapenzi makubwa na Qur'an Tukufu, khulka ambayo naye aliirithi. Mababu zake kumi wa nyuma walikuwa wamehifadhi Qur'an kwa moyo. Alijifunza Qur'an Tukufu kutoka kwa mama yake na kupata elimu kwa waalimu kadhaa katika jimbo la Punjab. Elimu yake ilikuwa nzuri kiasi hiki ya kwamba alichaguliwa kuwa Mkuu wa Shule huko iliyokuwa inafundisha katika Kiingereza. Baada ya miaka minne kutokana na kiu yake alianza kuzunguka majimbo mengi ya India akisaka elimu. Akiwa na miaka ishirini na mitano alifunga safari kwenda miji mitakatifu ya Makka na Madina kujifunza elimu ya Hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. kutenda ibada ya Hija. Katika harakati zake za kutafuta elimu alibahatika kukutana na waalimu mashuhuri na watawa ambao waliongeza elimu yake na kumuwezesha kuwa mtaalamu wa Qur'an Tukufu, lugha na utabibu. Hadharat Nurudin alisikia habari juu ya Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Masihi Aliyeahidiwa kutoka kwa watu na baada ya kusoma baadhi ya maandiko yake aliathirika sana. Mara baada ya hija alifunga safari ya kwenda Qadian wakati Masihi Aliyeahidiwa hajatoa madai yoyote ya Umasihi. Ile kumuona tu Hadhrat Nurudin, alitambau ukweli ambao anauwakilisha na akawa sahaba wake wa kudumu. Baadaye tarehe 27 Machi mwaka 1889, Masihi Aliyeahidiwa alipoanza kuchukuwa Baiat (kiapo cha utii) katika mji wa Ludhiana, Maulana Hadhrat Nurudin r.a. alikuwa mtu wa kwanza kufanya Baiat. Baada ya safari ya Qadiani aliamua kuacha kazi na kufanya makazi Qadian. Lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s. hakukubali ombi hilo. Mwaka 1892 huko Bhera alianza ujengaji wa Zahanati kubwa, baada ya ajira yake kama tabibu wa mfalme. Karibu ya kukamilika zahati yake alifanya safari fupi ya Qadian. Lakini wakati wa kuondoka ulipofika, Masihi Aliyeahidiwa a.s. alimuomba asahau kubisa mahali alipozaliwa na afanye Qadian masikani yake ya kudumu. Hivyo hakurejea Bhera. Huko ndiko kulikuwa kujitupa kwake na utii kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Katika Qadian Hadhrat Nurudin alianzisha zahanati na kutoa matibabu bure kwa maskini. Aliishi na Masihi Aliyeahidiwa a.s. na akajitolea maisha yake kuendeleza ujumbe alioleta Masihi Aliyeahidiwa a.s. Alifundisha Qur'an Tukufu na Hadithi kwa watoto wa Masih Aliyeahidiwa a.s. na pia aliwafundisha maelfu ya wanafunzi wengine. Baada ya kifo cha Masihi Aliyeahidiwa a.s. mwaka 1908, Hadhrat Nurudin alichaguliwa kuwa Khalifa wa kwanza.

Mwaka uliofuata alianzisha madrasa Ahmadiyya (shule kwa mambo ya dini) na akaweka jiwe la msingi la Masjid Noor. Gazeti la Jumuiya, Al-Fazal lilianza kuchapishwa wakati wa ukhalifa wake. Hadhrat Nuruddin alikuwa na nafasi ya pekee kwa sababu ya kuipenda Qur'an Tukufu na kumpenda Masihi Aliyeahidiwa a.s., imani thabiti juu ya Mwenyezi Mungu, Taqwa ya hali ya juu, na utumishi uliotukuka kwa binadamu. Mapenzi makubwa ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa Hadhrat Nuruddin yameelezwa katika ubeti wa Kiajemi kama ifuatavyo: "Ingekuwa vizuri kiasi gani kama kila mfuasi wangu angelikuwa kama Nuruddin." Hilo linawezekana tu kama kila nafsi imejaa yakini ya imani. Alifariki mwaka 1914. *Inna lillahi wa inna illahi rajiuun.*

-

HADHRAT MIRZA BASHIRUDDIN MAHMOOD AHMAD KHALIFATUL MASIH II

Hadhrat Mirza Bashiru-ddin Mahmood Ahmad r.a. alikuwa ni Khalifa wa Pili wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Alikuwa ni Khalifa mwenye sifa ya aina yake, kwani kuzaliwa kwake kulitabiriwa na mitume pamoja na watawa.

Juu ya haya Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipata alama za kimbinguni juu ya ukweli wa Islam kufuatia siku arobaini za maombi huko Hoshiarpur (India). Mwenyezi Mungu alimfunulia kwamba atapata mwana mwema na safi (Muslih Mauud) atakaye zaliwa katika kipindi cha miaka tisa. Alikuwa tayari amekwisha chapisha bishara hiyo tarehe 20 Februari, 1886 ambayo ilisema kijana huyu atakuwa na akili nyingi na uelewa mkuwa na atakuwa mpole wa moyo aliyejazwa elimu ya dunia na ya kiroho.

Tarehe 14, Machi 1914 baada ya kifo cha Khalifatul Masihi wa Kwanza r.a, Hadhrat Mirza Bashiru-dinn Mahmood Ahmad r.a. kwa sauti moja alichaguliwa kuwa Khalifatul Masih wa Pili, wakati huo alikuwa na umri wa miaka 25.

Chini ya uongozi uliotukuka wa Hadhrat Khalifatul Masihi II Jumuiya ya Ahmadiyya ilikuwa ya kupata maendeleo kwa mapana na marefu. Miaka yake 52 ya ukhalifa kilikuwa kipindi cha maendeleo makubwa ya Jamaat. Maendeleo yanayoonesha dhahiri msaada wa Mwenyezi Mungu.

Tarehe 12 Aprili, 1914 alizindua Majlis-e-Shoora ya kwanza katika ukhalifa wake iliyoweka mikakati ya kueneza dini ya Islam. Mwezi Disemba, 1923 sehemu ya kwanza ya maelezo ya Qur'anTukufu ilichapishwa miaka tisa baadaye. Tarehe 23 Septemba, 1923 alihudhuria mkutano huko Wembley, Uingereza ambako alitoa hotuba ambayo baadaye ilichapishwa katika sura ya kitabu na ilipewa jina *"Ahmadiyyat or the True Islam"* (Ahmadiyya, Uislam wa kweli). Tarehe 20 Mei 1928 alifungua Jamia Ahmadiyya (Chuo cha kufundishia wabashiri). Mwaka 1934 alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kashimir na alijitahidi sana katika utetezi wa watu wa Kashmir.

Aliandika vitabu vingi na miongoni mwa hivyo ni majarida kumi yenye maelezo ya kina juu ya Qur'ani tukufu. Wakati wa Ukhalifa wake matawi mapya yalifunguliwa katika nchi mbalimbali kama vile Ceylon na Mauritius katika mwaka 1915, Amerika katika mwaka 1920, Afrika Magharibi katika mwaka 1921, Indonesia katika mwaka 1925 na Falestina katika mwaka 1928.

Msikiti wa Alfadhil London, umewekwa jiwe la msingi katika mwaka 1924 na Khalifatul Masihi wa II r.a.

Ili kuongeza kasi ya mahubiri nje ya Pakistan, mpango mpya uitwao Tahrik-i-Jadid ulianzishwa, ambao ulijengwa kwenye kanuni kumi na tisa. Chini ya mpango huu, Waahmadiyya walitakiwa kuishi maisha ya kawaida na kujitolea zaidi kifedha na wakati wao kwa ajili ya kuendeleza mbele Islam. Pia walishauriwa kujifunza zaidi na kuwapatia elimu watoto wao. Matokeo ya mpango huu ni kwamba matawi zaidi yalifunguliwa katika nchi mbalimbali. Kama vile Afrika Masharki katika mwaka1934, Japan mwaka 1935, Burma mwaka 1938, Ufaransa katika mwaka 1937, Uhispania katika mwaka 1946, Uholanzi katika mwaka 1937, Uswizi katika mwaka 1948, Ujerumani Magharibi katika mwaka 1959, Denmak katika mwaka 1956. Baadaye vituo vingine vilifunguliwa huko Sweden, Norway, Kisiwa cha Fiji na Guyana Marekani ya

Endelea uk. 4

ALHAAJ MAULVI HAKEEM NURUDDIN - HADHRAT KHALIFATUL MASIH I

Na Seif Nakuchima,
Dar es salaam

Napenda kutoa maelezo yangu juu ya Hadhrat Alhaj Maulvi Nurudin, Khalifatul Masih wa kwanza. Qur'an Tukufu yasema kuwa Mashahidi (Manabii, makhalifa, na wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu) hawafi. Wanaendelea kuishi kadiri mambo waliyoyaanzisha pamoja na madhumini yake na mafanikio.

Warithi na wafuasi wao wanaendelea kuishi na kujitolea kwa dhati katika kutekeleza na kufanikisha madhumuni hayo.

Nimepewa jukumu la kumuelezea Khalifatul Masih wa kwanza. Lakini ninadhani ya kwamba sehemu ya maisha yeke kabla ya Ukhalifa ni muhimu pia kuielezea kwani sehemu hiyo pia ni kitabu chenye mafunzo yenye thamani kwetu tena yaliyo waziwazi.

Hadhrat Maulvi Nuruddin r.a. alizaliwa katika mji wa Bhera uliyoko katika wilaya ya Shahpur katika jimbo la Punjab mnamo mwaka 1841. Alikuwa ni mtoto wa mwisho katika familia yenye wavulana saba na wasichana wawili. Kwa upande wa baba yake, yeye ni kizazi cha 34 kutoka kwa Khalifa Omar r.a. Khalifa wa pili wa Mtume wa Islam Muhammad s.a.w. Baba yake aliitwa Hafidh Ghulam Rasul ambaye kwa uchache babu zake 10 walikuwa wamehifadhi Qur'an Tukufu.

Mama yake aliitwa bi Nuur Bakht aliyekuwa wa jamii ya A'waan inayopatikana maili chache kutoka Bhera. Mama huyu alikuwa akiwafundisha watoto wadogo wa jirani tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa Kipanjabi pamoja na taratibu za msingi kabisa za dini ya Kiislam (fiqhi). Mtoto wake wa mwisho pia alifundishwa naye.

Katika maisha ya baadaye kidogo Hadhrat Nuruddin alikuwa mara nyingi akisema aliisikia Qur'an ikisomwa na mama yake akiwa tumboni mwake na alinyonyea mapenzi ya Qur'an pamoja na maziwa ya mama yake. Baba yake pia alikuwa na mapenzi makubwa ya Qur'an Tukufu. Alikuwa tajiri ambaye alitumia kiasi kikubwa cha fedha kununua nakala nyingi za Qur'an Tukufu kutoka sehemu za mbali kama vile Bombay na kuzigawa bure.

Nuruddin alipokuwa mdogo alipelekwa shule. Nuruddin kwa msaada mkubwa wa Mwenyezi Mungu alipata busara kubwa sana katika maisha yake. Kaka yake mkubwa Maulvi Sultan Ahmad alikuwa na shauku na hivyo alichukuwa dhamana ya kumlea. Wakati huo Kiurdu haikuwa lugha ya kawaida katika Panjabi. Nuruddin alikisia kikizungumzwa kwa mara ya kwanza na askari kutoka Diyoband na alipenda sana lugha hii. Alikuwa na hamu kubwa ya kusoma vitabu vya Kiurdu na alipata faida kubwa kwa kusoma vitabu vilivyoandikwa na watu wa familia ya Shaah Walii Ullah wa Delhi. Alianza kuvipenda vitabu mapema sana hivyo kujikusanyia vitabu vingi.

Tangu wakati wa utoto wake alijiepusha na matumizi ya lugha ya kipuuzi na watoto wenziwe waliheshimu hili kila walipocheza naye. Alikuwa hodari wa kuogelea na alikuwa akienda kuogelea katika mto Jhelum hata wakati wa baridi kali. Alipofikia umri wa miaka kumi na miwili, siku moja alifuatana na kaka yake ambaye alikuwa na kiwanda cha uchapaji huko Lahore. Wakiwa Lahore Nuruddin r.a. alipata ugonjwa ambao alitibiwa vizuri sana na Hakimu Ghulam Distigiir wa Said Mitha. Baada ya kuridhishwa namna alivyotibiwa Nuruddin r.a. alipata hamu ya kusomea udakitari (utabibu).

Kaka yake alimbembeleza sana asome Kiajemi na alimwahidi katika hilo kwamba angemtafutia mwalimu mzuri na maarufu sana wa Kiajemi, Mushi Muhammad Qassim wa Kashmir. Mwalimu huyu alimfundisha Hadhrat Nuruddin kwa bidii, huruma na hekima kubwa kiasi kwamba baada ya muda mfupi Hadhrat Nuruddin alipata kiwango cha uhakika wa lugha hiyo. Kwa safari hii alikaa Lahore kwa miaka miwili. Baadaye alirudi Bhera ambako aliendelea na masomo yake ya Kiajemi kwa mwalimu aliyejulikana kwa jina la Haji MIyaan Sharif-udin. Baada ya siku chache kaka yake Maulawi Sultani Ahmad pia alirudi Bhera na alimwanzishia masomo yake ya kawaida ya Kiarabu. Alitumia njia iliyo rahisi sana ya kumfundisha ambayo ilimfanya apende sana na kuwa makini na hivyo ilimwezesha kuendelea vizuri sana katika kusoma lugha ya Kiarabu ambayo kwa wakati huo ilionekana kuwa ni lugha ngumu kidogo kwani wakati huo, Wapanjabi walikuwa wametoka kutawaliwa kisiasa na Waingereza ambao walishaharibu kabisa utamaduni wa kusoma Kiarabu.

Mwaka 1858 akiwa na umri wa miaka 17 alianza masomo ya Diploma ya Elimu katika shule ya Rawalpindi. Mkuu wa shule Maulawi Skandar Ali alipendezwa sana na maendeleo yake mazuri kiasi hiki kwamba aliweza kumsamehe



Maulana Hakeem Nuruddin Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

kuhudhuria baadhi ya vipindi darasani. Hadhrat Nuruddin r.a. alitumia muda huo wa msamaha kwa faida kwani alikuwa akijiimarisha kwenye masomo mengine ya nyongeza kupitia kwa walimu mbalimbali binafsi, na kwa kipindi cha miaka minne ya kozi alikuwa ameshakuwa mahiri katika masomo mengi sana. Alifanya vizuri sana katika mitihani ya diploma kiasi kwamba alipopata umri wa miaka 21 aliteuliwa kuwa mkuu wa Shule katika shule ya Pind Dadan Khan, mji uliyoko maili chache kutoka Bhera kwa kukatisha mto Jhelum. Alishikila cheo hicho kwa miaka 4.

Akiwa Pindi Dadan Khan aliendelea na mafunzo yake ya Kiarabu chini ya uangalizi wa kaka yake Maulawi Sultan Ahmad. Pia alianza kupata ndoto zenye ukweli ambazo zilisaidia sana katika kuimarisha maendeleo yake ya kiroho.

Kuacha kwake ukuu wa shule ilikuwa kama mchezo na mwenyewe alieleza hivi: "Ilitokea ya kwamba mkaguzi wa shule alikuja na akanikuta ninakula. Nilimkribisha. Badala ya kukaribia chakula au kukataa wito wangu, alianza kujibaraguza kwa kusema ninaona ya kwamba hujanitambua. Ninaitwa Khuda Barksh na ni mkaguzi wa shule."

Hadhrat Nuruddin r.a. akasema 'Oh!' bila shaka, vizuri kabisa! Wewe ni mtu mwenye heshima sana. Huwezi kula chakula anachokula mwalimu. Uzuri gani huo? Baada ya kusema haya niliendelea kula chakula changu, na yeye akiwa amemshika farasi wake, alisubiri mimi niwaambie wanafunzi wakamshikie farasi. Aliponiona sishughuliki, aliniomba: Tafadhali mwambie mwanafunzi aje kunishikia farasi.

Nilipomjibu bwana mkubwa umekua ni mtu mwenye hadhari kubwa kiasi hiki kwamba huwezi kula chakula alichokukaribisha mwalimu kwa maana ya kwamba itakuwa ni rushwa, sasa nitawezaje kumuomba mwanafunzi aje kukushikia farasi wako. Wanafunzi wanakuja shule kusoma na siyo kusaidia shughuli hizi za kuchunga. Hata hivyo, unaweza pia ukaomba farasi afungwe kamba na kulishwa. Itawezekanaje farasi alishwe na wewe mwenyewe hauko tayari kukubali ukaribisho wa mwalimu?

Wakati huu alionyesha ya kwamba angeendelea na kuwahoji wanafunzi ambapo niliwatayarisha katika utaratibu na mwenyewe nikajitoa na kusimama kando.

Mkaguzi alifanya mahojiano na wanafunzi baadaye akaniambia nimesikia ya kwamba una uwezo sana kiakili na una diploma ya daraja la juu sana ya elimu. Labda hiyo ndiyo inayokufanya kuwa na tabia yako hii ya kiburi.

Nilimjibu: "bwana mkubwa sithamini kipande mraba hichi chenye nchi chache za karatasi kama ninavyomthamini Mungu. Baadaye nilifuata diploma yenyewe nikaichana vipande vipande mbele ya macho yake na kuonyesha ya kwamba simshirikishi Mwenyezi Mungu na kitu chochote. Mkaguzi aliniomba radhi na kujilaumu kwa suala zima alilosababisha kupotea kwa diploma yangu. Ukweli ni kwamba kuichana diploma ilikuwa ni sehemu ya mapinduzi katika miaka yangu na ilifungua milango ya Rehema za kimbingu."

KUTAFUTA ELIMU

Kupata kwake uhuru baada ya miaka minne ya kufungwa katika kazi ya Mwalimu Mkuu, kijana Nuruddin akiwa na umri wa mika ishirini na tano alirudi kwenye mambo yake yaliyompendeza sana; kutafuta elimu. Baba yake alimuandalia kusoma Kiarabu kwa Mwalimu Maulawi Ahmad Din wa Bagguwala. Lakini kusoma kule ndani yake kulikuwa na mpango wa kujenga msikiti mkubwa na hivyo wanafunzi hawakuwa na budi ya kumfuata Mwalimu wao. Nuruddin alitumia mwaka wote katika shughuli hii ya nguvu na alijikuta kidogo anapata unafuu mwishoni mwa kipindi hicho, alimweleza kaka yake Maulvi Sultan Ahmad na kumkabidhi kwa Hakimu Muhammad Bakhsh na waalimu wengine. Siku chache baadaye wanafunzi wenzake walimbembeleza waende Rampur katika kutafuta elimu ya juu zaidi. Alipoeleza mpango huu kwa baba yake alikubali mara moja na akampa ruhusa. Lakini alimuusia katafute elimu ukiwa unafahamu zaidi ya habari tulizonazo ila usilitaje jambo hili kwa mama yako usije ukampa majonzi kwa kuchelea ya kwamba mtapoteana kwa muda mrefu sana na hivyo akakubembeleza usiondoke.

Wakati akijiandaa na safari alikumbuka ushauri aliokuwa akipewa mara kwa mara ya kwamba popote unapofika ni lazima utengeneze uhusiano wa kirafiki na mkuu wa mji, daktari mzuri, watu wenye utakatifu na wananchi wengine walio juu.

Akiwa na umri wa miaka ishirini na saba, Nuruddin aliondoka Lahore kwenda Rampur kwa miguu akiwa na watafuta elimu wenzake wawili. Safari ilikuwa ni nzito tena iliyochukuwa siku nyingi. Hakuna waliomfahamu huko Rampur. Katika kufika huko walifikia katika msikiti ambao ulikuwa kama umetelekezwa. Kwa siku mbili binti wa miaka 8 aliwaletea chakula asubuhi na jioni. Alipoleta chakula asubuhi ya siku ya tatu msichana yule alisema "mama yangu anawaomba mumuombee kwa ajili ya mumewe ili aweze kumfanyia mema." Hadhrat Nuruddin alikwenda na msichana yule nyumbani kwao na alimuomba baba yake kwa kutumia maneno mazuri yenye kubembeleza ambayo yalileta suluhu baina ya bwana yule na mkewe, ambapo udhihirisho wa Rehema za kimbingu ulionekana alitoa shukran kwa Allah.

Katika tukio moja kundi kubwa la wanafunzi walikuwa wakijadiliana juu ya tatizo fulani. Walipoliangalia kwa muda Hadhrat Nuruddin aliwatangazia ya kwamba analo jibu lake. Kundi kubwa la wanafunzi, wengi wao walimuhukumu kwa hali yake ya muonekano wa udumi, wakaanza kumdharau. Ila wanafunzi wa Kipanjabi walisimama kidete kutaka apewe nafasi ya kusilikilizwa ambayo ilikubalika. Alipendekeza ya kwamba mtaalamu wa sarufi achaguliwe ambaye anaaminika na asiye na upendeleo wa aina yoyote. Alichaguliwa Maulawi Ghulaam Nabii Sahib ambaye alifurahishwa sana na majibu ya Hadhrat Nuruddin r.a. na akamlinganisha na Maulawi ambayo ilikuwa ni sifa kwa kijana kama huyu.

Maulawi Nuruddin r.a. hakuridhika namna elimu ilivyokuwa ikitolewa kwa wakati huo. Kwani mwanafunzi aliachwa peke yake na hakupewa maelekezo stahiki na uangalizi

Itaendelea Toleo lijalo, Inshaallah.

KARNE MOJA YA UKHALIFA

Kutoka Uk. 2

kusini. Zaidi ya hayo misikiti mingi ilijengwa katika nchi tulizozitaja. Na Jumuiya ilivyokuwa inakuwa kwa haraka wanachama waligawanywa kufuatana na rika na jinsia kwa ajili ya utendaji mzuri. Tanzim (makundi) zifuatazo zilianzishwa: Lajna Imaillah, kwa wanawake waliozidi miaka 15 - ilianzishwa tarehe 25 Disemba 1922. Majlis Nasiratul Ahmadiyya kwa ajili ya mabinti walio chini ya miaka 15- ilianzishwa mwezi Februari, 1939. Majlis Ansarullah kwa wanaume walio na umri wa miaka arobaini kwenda juu, ilianzishwa Julai 26,1940. Majlis Khudamul Ahmadiyya kwa ajili ya vijana wenye umri wa miaka kumi na tano hadi arobaini, ulianzishwa tarehe 25 Disemba 1938. Majlis Atufal Ahmadiyya kwa ajili ya watoto wa miaka 7 hadi kumi na tano ulianzishwa Julai 26, 1940.

Kutoka Januari 28, 1944 Hadhrat Mirza Bashiru-ddin KHalifatul Masihi II alidai kwa mara ya kwanza kwa hakika kwamba yeye ndiye Mwana wa ahadi kama ilivyotajwa katika bishara inayomhusu 'Muslih Mauud' katika mikutano ya hadhara, aliiambia jamaat kwamba madai yake yalitokana na wahyi mbalimbali na njozi.

Tarehe 28 Disemba, 1957 alitangaza mpango wa kueneza mahubiri ili kuwafundisha na kuwapa elimu watu wa vijijini nchini Pakistan.

Khalifatul Masih wa II alikuwa na kipaji kikubwa cha uongozi, bingwa wa mipango, imani kubwa kwa Mwenyezi Mungu, ushujaa na bingwa katika nyanja mbalimbali na mvuto mkubwa. Hapana shaka uongozi wake wa miaka 52 ni kurasa tukufu katika historia ya Ahmadiyya.

HADHRAT MIRZA NASR AHMAD – KHALIFATUL MASIH III 1965 – 1982

Hadhrat Mirza Nasir Ahmad r.h.a alizaliwa tarehe 10 Novemba 1909. Kuzaliwa kwake kulielezwa katika ufunuo aliopewa Masihi Aliyeahidiwa a.s.:
"Nitakupa kijana ambaye atakuwa mjukuu wako". Hali kadhalika baba yake Khalifatul Masih II aliambiwa na Mweyezi Mungu kuwa angepewa mtoto ambaye atakuwa Nasir au msaidizi wa dini.

Hadhrat Mirza Nasir Ahmad rh.a alihifadhi Kurani Tukufu akiwa na umri wa miaka 13. Julai 1929 alipata shahada ya Maulvi Faadhil (Msomi wa dini) kutoka Chuo Kikuu cha Punjab. Mwaka 1934 alihitimu katika chuo Kikuu cha Lahore.

Alikwenda Uingereza kwa ajili ya Elimu ya juu Mwaka 1914, na Novemba 1938 alirejea Qadian baada ya kupata shahada ya uzamili (M.A.) kutoka chuo Kikuu cha Oxford Uingereza. Mara baada ya masomo yake alianza kuitumikia Islamu.

Kwanza alitumika kama Profesa wa masomo ya Kurani, na kisha mwaka 1939 mpaka 1944 alikuwa Mkuu wa Chuo cha Jamia Ahmadiyya katika Qadian.

Mei 1944 hadi Novemba 1965 alitumika akiwa Mkuu wa Chuo cha Taalimu - l - Islamu huko Rabwah, Pakistani.

Novemba 8,1965, wakati Khalifa wa Pili r.a. alipofariki huku Rabwah Pakistani, Hadhrat Mirza Nasir Ahmad rh.aalichaguliwa kuwa Khalifatul Masih III.

Kikao cha kumchagua Khalifa kiitwacho MAJLIS INTIKHAB KHILAFAT kilichompitisha kuwa Khalifa (kikao hiki au baraza hili la Uteuzi wa Khalifa kilianzishwa na Hadhrat Khalifatul Masih wa pili).

Katika kipindi chake cha Ukhalifa kilichochukua takribani miaka 17, alianzisha mfuko wa Fadhl

– Umar – ambao kutokana na mfuko huo – Pesa iliweza kutumika katika mambo ya Utafiti, kuinua elimu, kusaidia katika shughuli za mambo ya Mahubiri na kushughulika juu ya mambo ya Uchumi wa Jamaat. Chini ya mpango huo, maktaba ya kisasa kabisa ilifunguliwa mjini Rabwah.

Katika mwaka 1970, Hadhrat Mirza Nasir Ahmad alitembelea Afrika ya Magharibi ambako alitangaza mpango kabambe wa NUSRAT JAHAN ambao kwa ajili yake zilikusanywa pesa sawa na pauni ya Uingereza laki 1 (100, 000).

Pesa hizo zilitumika kuwakusanya madaktari, waalimu ambao watakaoweza kujitolea katika kuanzisha shule na hospitali, katika Afrika ya Magharibi kwa nia ya kutoa huduma kwa wanadamu bila ya kuwa na lengo la kupata faida.

Katika kipindi kifupi shule za sekondari 15 na hospitali zipatazo 17 zilifunguliwa katika Afrika ya Magharibi.

Katika mwaka 1973, Hadhrat Khalifatul Masih III alitangaza mpango mkubwa kabisa ambao haukuwa tu na uhusiano wa kutimia kwa miaka 100 ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Ahmadiyya, bali pia alianzisha mipango na taratibu ambazo zingefanywa karne inayofuatia.

Hii ilijumuisha kuanzishwa kwa vituo vipya katika nchi mbalimbali duniani ili kueneza Islamu kutoa tafsiri ya Kurani katika lugha mbalimbali, uanzishwaji wa viwanda vya uchapishaji na vituo vya redio. Kupitia mpango huu, misikiti ilijengwa katika nchi za Sweden, Norway pia kituo kikuu cha Jumuiya ya Ahmadiyya kilijengwa nchini Uingereza.

Ilikuwa ni wakati ambao jiwe la msingi lilipokuwa likiwekwa ndipo kauli mbiu ya ***MAPENZI KWA WOTE CHUKI SI KWA YEYOTE*** ilipoanzishwa.

Kuanzia Mei 29, 1974 vurugu za hali ya juu zilitokea dhidi ya Waislamu wa Ahmadiyya nchini Pakistani. Vurugu hizi kwa kiasi kikubwa zilipata nguvu toka Serikalini. Wakati huo kiongozi wa nchi hiyo alikuwa ni marehemu Zulfikar Alli Bhutto ambaye alikuwa Waziri Mkuu.

Nyumba za Waahmadiyya ziliporwa na kuchomwa moto, na Waahmadiyya wengi kwa hakika waliuawa katika vurumai hizo. Wanajumuiya wa Jamaat Ahmadiyya walitengwa kabisa na jamii.

Na wengi wa Waahmadiyya

waliokuwa watumishi katika ngazi za juu Serikalini, pia jeshini walilazimishwa kustaafu. Wakati wa kipindi hicho kigumu chini ya Uongozi wa Khalifatul Masih III rh.a, waliikabili hali hiyo, kwa subira, uvumilivu mkubwa na maombi.

Mwishowe Septemba 7, 1974, bunge la Pakistani likapitisha sheria kudai kuwa Waahmadiyya sio Waislamu. Kwa hakika jambo hili lilikuwa baya sana mbele ya Mwenyezi Mungu.

Matokeo yake ilikuwa ni mwisho mbaya sana kwa Waziri Mkuu wa Pakistani Zulfikhar Alli Bhutto kwani alipinduliwa kisha alifungwa jela na hatimaye alinyongwa kwenye tarehe 4 /04/1979.

Hadhrat Mirza Nasir Ahmad rh.a alifariki dunia mwaka 1982, baada ya kuitumikia Jumuiya ya Ahmadiyya kwa muda wa miaka 17 ambapo namna yake ya Uongozi na ujuzi wa Utawala ulileta mafanikio makubwa katika Jumuiya ya Ahmadiyya.

HAZRAT MIRZA TAHIR AHMAD – KHALIFATUL MASIHI WA NNE 1982 – 2003:

Hazrat Mirza Tahir Ahmad, Khalifatul Masihi wa nne alizaliwa katika mwaka 1928. Alipata elimu yake katika India na chuo kikuu cha London, nchini Uingereza. Alichaguliwa kuwa Khalifatul Masihi wa nne tarehe 10 mwezi wa sita mwaka 1982. Mwishoni mwa mwezi wa saba katika mwaka 1982 – Hazrat Khalifatul Masihi wa nne alitembelea Ulaya kwa ajili ya ukaguzi wa vituo vya Ahmadiyya vilivyopo nchi za ng'ambo. Wakati wa safari yake – Huzur alifungua vituo viwili katika Uingereza na akaanzisha MAJLIS SHOORA (baraza la majadiliano, katika nchi nyingi. Pamoja na kuendesha vipindi vingi vya maswali na majibu (MAJALIS IRFAN) katika nchi zote alizotembelea, pia alifanya mikutano 18 na waandishi wa habari vile vile alihutubia katika mji wa Zurich, Switzerland.

Tarehe 10 mwezi wa tisa mwaka 1982 – Khalifatul Masihi IV rh.a alifungua msikiti wa kihistoria wa Basharat katika mji wa Pedroabad nchini Uhispania. Msikiti huu ni wa kwanza kujengwa katika kipindi cha miaka 700, baada ya kuanguka dola ya Kiislamu huko Uhispania.

Tarehe 30 mwezi wa tisa mwaka 1983 alitembelea Australia ambako aliweka jiwe la msingi kwa ajili ya msikiti wa kwanza wa Kiahmadiyya katika Australia.

Hazrat Mirza Tahir Ahmad rh.a alianzisha mipango mingi kwa

ajili ya kuhimiza na kupeleka mbele Uislam duniani kote. Katika mipango hiyo pia ilihimizwa kwa Waahmadiyya kujifunza lugha ya Kihispania na kuwashauri wale wote waliostaafu kutumia muda wao wote uliobaki kuitumikia Islam.

Mpango mwingine, mwito katika njia ya Allah ulianzishwa, ambao ulimtaka kila Muahmadiyya kuhubiri kwa marafiki zake, pia wote wale alio na ukaribu nao katika hotuba zake mbali mbali, Khalifatul Masihi wa nne alifundisha na kutoa ufafanuzi wa namna gani mahubiri yafanyike.

Mpango huu ulileta mafanikio makubwa tokea ulipoanzishwa.

Tarehe 3 mwezi wa nne mwaka 1987, Khalifatul Masihi IV rh.a alianzisha mpango mwingine unaoitwa WAQFU NAU – ambao uliwataka Waahmadiyya wawatoe watoto wao wakfu kuitumikia Jamaat, kwa wale wote, ambao watoto wao waliozaliwa kabla ya tarehe 23 mwezi wa tatu mwaka 1989 – ambao kimsingi tarehe hiyo inaonesha kutimia kwa karne moja tokea ilipoanzishwa Jumuiyya ya Ahmadiyya.

Kipindi cha mpango huu kilirefushwa toka miaka miwili mpaka miaka minne. Lengo la watoto 5000 liliwekwa ili waje kuitumikia Jumuiyya katika karne ijayo na kueneza Islam duniani kote.

Pamoja na kuzuka vurugu na ghasia katika vipindi viwili tofauti katika Pakistan – yaani mwaka 1953 na 1974, Jumuiyya hii iliyoanzishwa kwa nguvu ya Allah iliendelea vizuri katika vipindi vya Khalifa wa pili na wa tatu. Kwa kuona mipango madhubuti na imara iliyoanzishwa na Khalifa wa nne (Mirza Tahir Ahmad) serikali ya Pakistan ikishirikiana na Waislam wa kisuni walio wengi ikaanzisha mateso na madhila dhidi ya Waahmadiyya. Baadae kidogo likatolewa tamko rasmi la serikali tarehe 26/04/1984 la kuwakufurisha Waahmadiyya. Jinsi ilivyozidi kuwa vigumu kuulinda Ukhalifa katika Pakistan sawa na sheria zilizowekwa ilimlazimu Khalifa wa nne kuhamia Uingereza katika mwaka 1984. Uhamaji wake ulifungua ukurasa mpya katika historia ya Jumuiyya ya Ahmadiyya.

Hazrat Mirza Tahir Ahmad rh. a alimtaka rais Zia – ul – Haq na wafuasi wake waingie katika mubahala. Hii ikiwa na maana ya kwamba kumuomba Mungu Apitishe hukumu yake – na ni dhahiri kabisa Mungu Atamuadhibu vibaya yule aliye muongo.

Huzur pia alisema ya kwamba Mungu Atamuadhibu Zia ul haq japokuwa Zia ul haq hatofuata taratibu za mubahalla.

Matokeo yake, juu ya mubahala yakaja kuwa mabaya sana kwa Zia ul haq na wafuasi wake. Maana Zia ul haq na wafuasi wake waliuawa katika ajali ya ndege, ambayo mpaka leo haijulikani chanzo chake kilikuwa ni nini?

Kwa hiyo basi kwa mara nyingine Mungu Ameonyesha ukweli juu ya Ahmadiyya kwa kumuadhibu yule aliye muongo chini ya uongozi wa Hazrat Mirza Tahir Ahmad.

Msikiti mkubwa katika Amerika ya kasikazini (Baitul Islam) ulijengwa Toronto – Canada katika mwaka 1992, na mwaka 1994 msikiti mwingine uitwao 'Baitul Rahman' ulifunguliwa katika Mji wa Washington DC - Amerika na ilikuwa ni katika kipindi cha Khalifa wa nne ambapo "Muslim Television Ahmadiyya" (MTA) ilianzishwa. Hazrat Mirza Tahir Ahmad alifariki mwaka 2003, Uingereza.

MIRZA BASHIRU-DIN MAHMOOD AHMAD: HADHRAT KHALIFATUL MASIH II R.A.

Mfasiri: Suleiman Kagobe

Ili kufahamu uhodari wa mtu ni vema kuangalia ni jinsi gani anavyokabiliana na msukosuko katika maisha yake. Au matatizo yanapo tokea kuhusu jamii yake ambayo na yeye ni miongoni mwao. Tukiwa tumeiweka kanuni hii akilini tunapoangalia maisha ya Khalifa wa pili tunaona tokea akiwa mdogo kabisa aliweza kukabiliana na misukosuko mikubwa ambayo kwa mtu asiye na moyo thabiti asingeweza kuyahimili.

Moja ya msukosuko uliyompata Khalifa wa Pili - ulitokea mapema na ulipelekea Jumuiyya ya Ahmadiyya igawanyike.

Ilikuwa ni baada ya kifo cha Masihi aliyeahidiwa, ndipo jambo hili lilianza kujitokeza - ilichukua takriban miaka sita kwa jambo hili kufahamika hadharani. Ilikuwa ni dhahiri shahiri kabisa kwa mtu yeyote yule aliyekuwa akifuatilia vizuri, mambo jinsi yalivyokuwa yakienda ndani ya Jumuiyya ya Ahmadiyya, katika mwaka 1903 - 1914 mambo yalikuwa yakienda mrama. Na muhusika mkuu wa tukio hilo la kugawanyika kwa Jamaat si mwingine ila ni Maulvi Mohamed Ally.

Suala kubwa lililokuwa limeikabili Jamaat ni kutaka kuelewa kikweli kweli ni nani hasa anapaswa kuwa ni mrithi wa Masihi Aliyeahidiwa sawa na wasia usemavyo.

Mohammed Ally na watu wake walishikilia ya kuwa alilipa uwezo mkubwa na wa juu, pia wa mwisho Baraza la Udhamini la Sadr Anjuman Ahmadiyya. Tatizo hili lilileta tabu sana mpaka Khalifa wa kwanza akaingilia kati ili kupunguza kasi yake.

Kwa hiyo aliitisha mkutano wa kihistoria tarehe 31/01/1909 ambao katika mkutano huo wajumbe kutoka kila Jamaat ya India, waliombwa kuhudhuria.

Huu ulikuwa ni wakati ambao aliona ya kwamba iwapo wale wanaoleta fikra za mgawanyiko wasiposhughulikiwa basi Jumuiyya ya Ahmadiyya na vyote ilivyovifanya na kuamini vitasambaratika.

Kwa hiyo basi akiwa na mtazamo wa mbali na jitihada bila ya kukata tamaa pamoja na maombi ya hali ya juu kwa ajili ya umoja na mafanikio ya Jamaat, alianzisha Anjuman Ansarullah katika mwaka 1911, ambayo ilihakikisha kila aina ya upinzani unaotaka kuvuruga taratibu ya Ukhalifa katika Jumuiyya unashindwa. Mafanikio ya kuweza kutatua matatizo ya ukhalifa ndani ya Jumuiyya ilikuwa ni moja ya mafanikio makubwa ambayo kwa kweli kila muahmadiyya anayohaki ya kujivunia. Na kumshukuru Mungu kwa dhati kwa kuweza kutupatia Khalifa Mtukufu kama huyu.

Kisha baada ya haya, uimarishaji wa Jamaat chini ya uongozi wake Imara, ni kipimo kingine cha uwezo na jinsi alivyokuwa mahiri katika nyanja ya utawala. Umoja na Mshikamano uliojengwa na Masihi Aliyeahidiwa na kuhuishwa zaidi na Khalifa wa kwanza. Yote hayo yalitakiwa kuendelezwa na kuimarishwa baada ya kifo chake ili kazi au ujumbe aliotumwa nao Masihi Aliyeahidiwa uende mbele. Na haya katika akili na fikra za watu waliokuwa hawaitakii mema Jamaat halikuwa ni jambo rahisi. Akiwa na wazo moja tu, la kujenga na kuimarisha, Hadhrat Amirul - Muumineen II alikusanya nguvu zake zote katika uimarishaji wa Jamaat.

Mpango wa NAZARAT aliounzisha 1918 ulifungua milango ya kuweza kuufanya Uislam (Ahmadiyya) kuenea katika pembe nne za dunia.

Ili jamaat iweze kueleweka kwa kiwango cha juu Hadhrat Khalifatul Masih II r.a. alianzisha mpango wa Tahrik Jadid ukiwa na masharti kumi na tisa. Na pia alianzisha Khudamul Ahmadiyya katika mwaka 1938, vile vile akaanzisha mpango wa Majlis Mushawarat tokea mwaka 1922. Kutokana na maamuzi yote haya Jumuiyya ilipiga hatua kubwa kuelekea kwenye mafanikio ambayo Mwenyezi Mungu Al-imuahidi Seyyidna Ahmad (a.s) Jumuiyya hii imekuwa na ushawishi mkubwa sana duniani na ni Jumuiyya hii pekee ambayo inaweza ikaibadilisha dunia na kuwa ni mahali bora kwa maisha ya mwanadamu. Sawa na ilivyobashiriwa na Masihi Aliyeahidiwa. Ili kufikia lengo hili, safari ya kulifikia lengo imekuwa ni ngumu na iliyojaa misukosuko.

Siri ya mafanikio makubwa ya mtu huyu mashuhuri yanaweza kufahamika kupitia ubashiri huu mkuu wa Masihi Aliyeahidiwa alioutowa kwa dunia kabla ya kuzaliwa kwa Hadhrat Mirza Bashiruddin Mamood Ahmad.



Hadhrat Mirza Bashiruddin Hadhrat Khalifatul Masih II r.a.

“Habari njema kwako, mtoto mzuri na muadilifu wa kiume atatokana nawe, amepewa roho mtakatifu, ni nuru ya Mungu, pamoja naye ni Fazal ambaye atakuja naye - utukufu mkubwa, mali nyingi itaambatana naye. atakuja duniani na atawaponya wengi kwa kutumia nguvu ya Kimasihi aliyonayo. Pamoja na baraka za roho wa kweli. Yeye ni neno la Mungu, kwa sababu ya huruma na ghera ya Mungu - Amemtuma na neno tukufu. Atakuwa na akili nyingi na atakuwa amebarikiwa na uelewa mkubwa (au akili nyingi) - kuja kwake kutabarikiwa sana na itakuwa ni onyesho la utukufu wa mbinguni - mwanga wa kiroho unakuja, mwanga wa mbinguni - Mungu Amempaka, Amempulizia utukufu wake. Tutampulizia roho yetu, atakuwa chini ya ulinzi wa Mungu - atakuwa haraka sana. Wafungwa na watumwa watapata uhuru wao kupitia katika mikono yake. Sifa zake zitaenea katika pembe zote za dunia, Mataifa yatabarikiwa kupitia kwake.”

BARAKA ZA UKHALIFA:

Tunasoma katika suratil Nur aya ya 56 inayotoa maelezo juu ya ukhalifa(24:56). Sawa na aya hii ahadi ya ukhalifa ipo wazi, bila ya kujificha na kwa kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) ni kiongozi pekee kwa binadamu wote ulimwenguni - Ukhalifa wake pia ni lazima uendelee mpaka mwisho wa dunia.

Hii ni moja ya tofauti kubwa ya ubora baina ya Mtume Muhammad (s.a.w) na mitume wengine.

Khilafat ni utawala wa kiroho wa Allah na uanzishaji wake hauhitaji mambo yoyote ya kisiasa (siasa haihitajiki katika kuuweka) Ukhalifa.

Wakati Ukhalifa ukiwa umewekwa na Mungu, umekuwa ukipatikana kupitia kwa Nabii wa Allah historia inatupa mifano mingi ya jinsi siku zote Ukhalifa unavyotanguliwa na Unabii na hakuna mfano hata mmoja ambao Ukhalifa unatokea bila ya kutanguliwa na Unabii.

Ukhalifa uloahidiwa ndani ya Qur’an Tukufu upo katika nyayo za Nabii, Mtume Mtukufu (s.a.w) anakariri wa akisema; “Unabii au Utume utabakia nanyi sawa na Mungu Atavyopenda, Yeye (Mungu) Ataufikisha katika mwisho wake na Ataufatisha na sawa na Atakavyopenda na kisha kuufikisha katika kikomo chake. Kisha Ufalme wa kikatili utafuatia, utadumu sawa na Mungu Atakavyopenda na mwisho kufikia kikomo chake. Kisha baada ya hapa utafuata utawala wa muelekeo wa kifalme sawa na Mungu Atakavyopenda na utafikia mwisho wake sawa na atakavyoamuru. Kisha utafuatia Ukhalifa baada ya Unabii”. (Musnad Ahmad).

Kutokana na ubashiri huu wa Mtume Muhammad (s.a.w) ni wazi kwamba UKhalifa utakaofuata baada yake utakuwa ni wa aina mbili na utafuatia mara tu baada ya kifo chake na kati ya Ukhalifa ule wa kwanza na wa pili - utaingiliwa na tawala za kikatili na ukandamizaji.

Mara baada ya kifo cha Mtume (s.a.w), utawala (uongozi) uliobarikiwa wa Ukhalifa ukafuatia kama ilivyobashiriwa, na ukasimamishwa tena mara baada ya kufika Masihi aliyeahidiwa na mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya ya waislam wa Ahmadiyya.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian alikuwa ni mtumishi mtiifu wa Mungu na mfuasi imara wa Mtume Muhammad (s.a.w). Alidai ya kwamba ametumwa n a Mungu mwenye nguvu kama muonyaji wa zama hizi, n a kwamba yeye ni Masihi aliyebashiriwa katika hadithi za Mtume (s.a.w) na pia ni Mahdi aliyemuelezea katika maneno yake. Alidai ya kuwa bashiri zote zinazopatikana katika vitabu vya dini tofauti kuhusu kutokea kwa Mjumbe wa Mungu katika siku za mwisho, bashiri zote zimekamilika katika dhati yake. Mwenyezi Mungu Amemwinua ili auhami na kuufundisha Uislam katika zama zetu pia Mwenyezi Mungu Amemjalia uwezo mkubwa wa kuijua Qur’an Tukufu pia Amemfunulia maana za ndani kabisa za Qur’an na ukweli. Kwa kazi yake ujumbe wake na mfano wake alimtukuza sana Mtume s.a.w na akaonyesha ubora wa Islamu juu ya dini nyingine zote, kiasi kwamba Mtume Muhamad s.a.w. aliweza kukubalika ya kuwa yeye ni mbora wa Manabii, kwa watu wa dunia nzima.

Wakati ambapo fikra za ushabiki wa dini, kutojali kabisa Imani na dini za watu wengime na kujaribu kuzifuta kwa namna yeyote dini nyingine, zilikuwa zimetawala fikra za Waislamu. Aliwaonyesha wale waliokuwa wakitafuta ukweli, Elimu nyingi na pana, Hekima na falsafa ya Qu’ran Tukufu. Hekima na mambo mengi ya kiroho yaliyofundishwa katika Qu’ran Tukufu na yakaoneshwa kwa ukamilifu wake na Mtume s.a.w. - yalionyeshwa tena na Masihi aliyeahidiwa, ili watu waweze kunufaika tena siyo tu kwa maneno yake bali pia kwa vitendo vyake (Kwa mfano wake).

Alipofariki Tanzia kutoka kwa waislam walio na fikra huru na wale wasio waislam walizieleza kwa heshima na taadhima sifa zake za kimasihi alizokuwa nazo, kwa mfano usafi wa moyo na uadilifu. Hata hivyo wapinzani, wasiokuwa na fikra nzuri walifurahia kifo chake wakiamini ya kuwa kila walichoamini ni kufru kubwa sasa kitakuwa kimekufa na kilichobaki itakuwa ni History.

Katika wakati huu muhimu, mfuasi wake barabara, mchamungu wa kweli na tabibu mtawa aliye na utambuzi mkubwa, na mtaalam pia mhadhiri wa Qur’an Tukufu kwa sauti moja alichaguliwa kuwa ni Khalifa wa kwanza wa Masihi aliyeahidiwa, kwa baraka za Mwenyezi Mungu katika nafasi hiyo aliweza kuliongoza jahazi la Ahmadiyya kwa usalama na kulilinda lisivunjike na dhoruba, jina lake ni Nurudin - likiwa na maana ya Nuru ya Imani, jina lake linalingana na huduma anayoitoa katika kuihudumia dini. Hadhrat Maulvi Nurudin alikuwa na imani hai juu ya Allah, Mwenye nguvu na alimtegemea Mungu pekee kwa mahitaji yake yote, kama Masihi wa Khalifa kazi zake zilikuwa nyingi na tofauti tofauti, pamoja na hali yake ya afya kuwa haitabiriki - alijitahidi kufanya kazi akiwa katika hali ya utulivu, bila ya kuonyesha kama ana maumivu na akionyesha jitihada ya kweli katika kazi yake.

Itaendelea Toleo lijalo, Inshaallah.

BUSTANI YA WASHAIRI

Watunzi waadhimisha Karne moja ya Ukhalifa

KARNE YA UKHALIFA, SHANI YA AHMADIYYA

1. Kwako ninakimbilia, Ewe mwenye kila sifa,
Nakuomba nipokea, ona nilivyo dhaifa,
Niweze kuisifia, karne ya Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

2. Shani ya Ahmadiyya, Karne ya Ukhalifa,
Umri miaka mia, imara bila ya nyufa,
Haijapata tokea, kwa umma wa Mustafa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

3. Zama zilipowadia, za yalotajwa maafa,
Wengi walipodhania, Islam ni ulofa,
Mola Akakadiria, kukuza yake sharafa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

4. Ndipo akamteua, Ghulamu alo nadhifa,
Elimu kamshushia, akampa na wadhifa,
Apate ongoza njia, kusherehesha suhufa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

5. Mirza akanadia, kuyaita mataifa,
Mimi ndiye Masihia, njooni mupange safa,
Akazidi shadidia, Yesu ameshatawafa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

6. Kuaga kwake dunia, hakukuwa kwa kifafa,
Aliandika Wasia, wenye njema taarifa,
Mola Ameniambia, musubiri Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

7. Wale walotegemea, Silsila itakufa,
Mara wakashuhudia, nguvu za Mola Raufa,
Kwenye nyayo za Nabia, ukaota Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

8. Nuruddin awalia, akavishwa Ukhalifa,
Akaivusha Jamia, kwenye kubwa taklifa,
Nuhusi ikakimbia, kuupisha Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

9. Bashirudin thania, kaupamba Ukhalifa,
Kaijenga Jumuia, kwa makubwa maarifa,
Nidhamu katuwachia, ili tubaki Hanifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

10. Nasir alotulia, mhifadhi Msahafa,
Nafasi ya thalathia, kauhami Ukhalifa,
Bunge la kijahilia, likagubikwa kashifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

11. Twahir arbaia, kaukuza Ukhalifa,
Ikashamiri Jamia, mikoa hadi tarafa,
Wapinzani kina Zia, wakadondoshwa ghorofa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

12. Masroor Khamsia, tuliyenaye Khalifa,
Ayyadahu Naswria, mambo yawe ashrafa,
Tuzidi itumikia, dini ya Mola Latifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

13. Leo twasherekea, karne ya Ukhalifa,
Matunda twajivunia, Jannati Alfaafa,
Sote tunashukuria, neema ni Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

14. Jamaat Ahmadiyya, hoja yetu Ukhalifa,
Nyoyo zitele khushua, roho zetu ni Arafa,
Ziko safi zetu nia, watulinda Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

15. Jamaat Ahmadiyya, ngome yetu Ukhalifa,
Wenyewe twajichangia, milioni za sarafa,
Mola Ametuokoa, watutosha Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

16. Dini twaipigania, Jemedari Ukhalifa,
Idara za Tarbia, Ishaat na Tasnifa,
Ewe mtafuta njia, njoo kwenye Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

17. Ummati Muhammadia, uzima ni Ukhalifa,
Wapi mtakimbilia, muipate takhfifa,
Ndwele mnazougua, dozi yake Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

18. Dini ya Islamia, umoja ni Ukhalifa,
Kugombania ulua, na vipando vya masofa,
Fujo zitaendelea, kwa kukosa Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

19. Aloahidi Jalia, kuuleta Ukhalifa,
Kwa waliominia, na vitendo insafa,
Kama wetu ni kuzua, anzisheni Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

20. Karne tunaishia, *zindabad* Ukhalifa,
Sisi na wetu dhuria, tuandame Ukhalifa,
Ije mia kisha mia, upevuke Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

Abdulrahman M. Ame,
S.L.P. 376, Dar es Salaam.

YATIMIZA JUMUIYA KARNE YA UKHALIFA

1. Kila njema nazo sifa, na mitume kufatia,
Ulioleta sahifa, na mitume kufatia,
Kadhalika ukhalifa, nyuma kuandamia,
Yatimiza Jumuiya, karne ya ukhalfa.

2. Karineya ukhalifa. yatimiza Jumuiya,
Waminio na malofa, nibudi kuitikia,
Tembea kwatakhlifa, theluji kuifikia,
Yatimiza Jumuiya, karne ya ukhalifa.

3. Ahadi ya ukhalifa, Allah kaikusudia,
Wa kwanza kupatadhifa, Adamu akaanzia,
Malaika wakatufa, Ibilisi katimua,
Yatimiza Jumuiya, karne ya ukhalifa.

4. Mtukufu Mustafa,Muhamadi katangoa,
Waminio wasolifa, walohai kwa Jalia,
Watakuwa kama tufa, nema hii kupokea.
Yatimiza Jumuiya, karne ya ukhalifa.

5. Hadithi ya Mustafa, mbingu imemuinua,
Ni nuru iliyo nadhifu, mwezi nyota kupambia,
Siyo shirikala fifa, kwamba utalizuwia,
Yatimiza Jumuiya, karne ya ukhalifa.

6. Mfano huu gorofa, tazidi kunyenyekea,
Ni Ahmad khalifa, Masihi wake Rasua,
Aitakasa suhufa, na dini Isilamia,
Yatimiza Jumuiya, karne ya ukhalifa.

7. Wakorofi masharifa, na mashehe kuchangia,
Wenye imani za nyufa, shetani kuwaingia,
Kila mara wachachafya, kuipinga jumuiya,
Yatimiza Jumuiya, karine ya ukhalifa.

8. Wapingaji mataifa, ukhalifa kupindua,
Wakajipanga wa safa, na vyeo kujipangia,
Mola mwenye maarifa, kaburi kawachimbia,
Yatimiza Jumuiya, karine ya ukhalifa.

9. Masihi huyu sekafa, wa Kadiani India,
Tatiwa nyingi kashifa, wafuasi kuuliwa,
Allah ndiye wakerefa, ushindi tampatia,
Yatimiza Jumuiya, karne ya ukhalifa.

10. Baada ya mufawafa, Ahmadi Mashihia,
Wapenzi wake Latifa, huzuni kuwaingia,
Nidhamu ndiyo yao sifa, walizidi kutulia,
yatimiza Jumuiy, karine ya ukhalifa.

11. Kadhihiri Al-Haji, Nurudin Hakimia,
Alopambika kwa taji, Masihi kumtambua,
Khalifa muongozaji, wa kwanza Ahmadiyya,
Yatimiza Jumuiya, karine ya ukhalifa.

12. Hakimu kainuliwa, peponi kenda tulia,
Kafika mtarajiwa, mwana aloahidiwa,
Bashiri dini mtawa, wafalume kumuitikia,
Yatimiza Jumuiya, karine ya ukhalifa.

13. Watatu ndiye Nasiri, nyota iliangazia,
Walojipanga kwa shani, na wanafiki sawia,
Kwa nguvu zake Kahari, moto ukawawakia,
Yatimiza Jumuiya, karine ya ukhalifa.

14. Wanne ni profesa, Tahiri Ahmadiyya.
Wasomi aliwatesa, kwa hoja za fizikia,
Na wahuni kuwaasa, Wisilamu kuchezea,
Yatimiza Jumuiya, karnine ya ukhalifa.

15. Wa tano kwa ukhalifa, Msasururi kuvutia,
Yu hai bado hajafa, yu-mzima wa afia,
Njoo ujipange safa, safinani kuingia,
Yatimiza Jumuiya, karine ya ukhalifa.

16. Twakushukuru Mwenenzi, kama Nabi Zakaria,
Mola wetu Azizi, maombi yetu pokea,
Wenye roho za masizi, hao waonyeshe njia,
Yatimiza Jumuiya, karine ya ukhalifa.

17. Awaita Ahmadi ni vema kumwitikia,
Ipandeni kwa juhudi, safina yake ingia,
Aridhi iwe shahidi, na ndipo itatulia,
Yatimiza Jumuiya, karine ya ukhalifa.

Kainuza H.R. Mbambwa, (Wa Ujiji),
S.L.P. 376, Dar es Salaam

SISI TUMEBAHATIKA

1. Ukhalifa ni alama, ya watu washika dini,
Wae wtendao meme, walojazika imani,
Amewataja Karima, wamo kwenye Kuraani,
Sisi tumebahatika, tunatimiza karine.

2. Watu hao wale wema, hasa walio kundini,
La Mtume akrama, Muhammad muhisani,
Watapewa kiti chema, Kurusiyu ya Manani,
Sisi tumebahatika, tunatimiza karine.

3. Wale wenye sifa njema, zenye nuru yambinguni
Ukhalifa kwao neema, itaodumu kundini,
Kundi halendi mrama, wao wanaye rubani,
Sisi tumebahatika, tunatimiza karine.

4. Twaimba tumesimama, sauti zenda mbinguni,
Twamuhimidi Karima, kwa furaha za moyoni,
Ukhalifa mti mwema, kwenye hii bustani,
Sisi tumebahatika, tunatimiza karine.

5. Wa kwanza ulinyauka, mti ule sa Adeni,
Matawi yalivunjika, mengi kuanguka chini,
Kwa mapenzi ya rabuka, umechipua mwishoni,
Sisi tumebahatika, tunatimiza karine.

6. Mti sasa watajika, uliota Kadiani,
Sana umenawirika, kila nchi duniani,
Ni wapi haujafika,mti huo nambieni,
Sisi tumebahitika, tunatimiza karini.

7. Mahadi alishafika, mnaye mngoja nani?
Alikuja kusimika, Ukhalifa wa zamani,
Ule ulio fujika, ulonyongeka vitani,
Sisi tumebahatika, tunatimiza karine.

8. Muoneni Nurudini, Khalifa alotukuka,
Amiri muuminin, sana alokubalika,
Wa kwanza kuwakundini, na wa kwanza kuongoka,
Sisi tumebahatika, tunatimiza karine.

9. Mirza Bashirudini, kamba ile alishika,
Akawa mtu wa thani, ukhalifa kuushika,
Msomeni vitabuni, yawatokeni mashaka,
Sisi tumebahatika, tunatimiza karine.

10. Wa tatu ndiye, Nasiri, khalifa wa kutajika,

Bhutto alipojasiri, kwa yeye alifutika,
Lililo baki kaburi, hayupo amezimika,
Sisi tumebahaitka, tunatimiza karine.

11. Twahir ni kamba nenen, kamba isiokatika,
Kawa khalifa na nne, kwake Zia atanyofoka,
Aliyhaona mavune, ndege ilipo anguka,
Sisi tumebahatika, tunatimiza karine.

12. Kaditama mhariri, Mikila apa nakoma,
Salamu kwa Masruri, khalifa wetu wa zama,
Huyu ndiye Jemedari, kwa yeye tupo salama.
Sisi tumebahatika, tunatimiza karine.

Ustadhi Abdul-Rahman Mikila, Morogoro

LEO IMEKAMILIKA

1. Alhamdulillahi, twamshukuru Jalia,
Kufikia siku hii, ya karine ya Rasua,
Ni mingi miaka hii, mia moja yatimia,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

2. Elfu mbili na nane, mwezi mei nakwambia,
Tarehe mbili sabaa, nakulomba ongezea,
Na uipate bayana, tupate kufurahia.
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

3. Kwa jina lake Rabana, leo tunashuhudia,
Na yeye ni wetu Bwana, uwezo katujalia,
Twakamilisha dhamana, Mola aloahidia,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

4. Na ukhalifa jamani, ni nema yake Jalia,
Ahadi alibaini, ninyi nyote mwaijua,
Ndani yake Kur'an humo katuelezea,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

5. Hadithi za Muhammad, pia zatuelezea,
Hamna katu unabii, sipokuwa ukhalifa.
Zingine zimebaini, hayo hayo wasikia,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

6. Mtume ni Muhammad, ahadi alipokea,
Kutoka wetu Manani, ukhalifa ukanzia,

Mtume alifariki, neema ikaanzia,
Leo imekalika, karine ya ukhalifa.

7. Yatupasa uturahi, kwa simu ya ukhalifa,
Katuruzuku Manani, ukhalifa kufikia,
Utulivu tushiriki, bila ya kero kutia,
Leo imemilika, karne ya ukhalifa.

8. Wa kwanza kwa Muhammadi, Abubakari anzia
Khalifa wake wa pili Umar nakutajia,
Watatu ni Uthumani, bin Afari elewa,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

9. Khalifa wake mwingine, ni Ali bwana sikia
Kaashika nambari nne, na hilo bwana elewa,
Hakuna tne mwingine, wakawa wamefikia,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

10. Muda mwingi ulipita makhalifa kujifia,
Kukawa wingi utata, vurugu zikatokea,
Mashehe wanza matata, kuwapoteza insia,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa,

11. Masihi wa Muhammadi, duniani kaingia,
Si mwingine ni Ahmad, huyu aliahidiwa,
Na Mola wetu Wadudi, kuwa tutampokea,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

12. Mjumbe ni wa Manani, tabiri kuelezea,
Kifo changu duniani, magizo nitawachia,
Kawaida ya Manani, ukhalifa kwendelea,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

13, Moja tisa sifuri nane, alifariki dunia,
Nurudini Muhisani, ukhalifa akapewa,
Akawa ni namba wani, wa Masihi Maridhia,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

14. Nakutajia wa pili, Mwana Muhahidiwa,
Mirza Bashirudini, huyu alishikilia,
Kwa kifo cha Nurudini, kilipo muwasilia,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

15 Mengi aliyabaini, ya ndani ya Jumuiya,
Ujumbe wake Masihi, duniani ni kuenea,
Tukapata hadi hasi, Mashariki Afrika,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

16. Na Nasiri Ahmadi, wa tatu huyu sikia,
Wa nne nam'baini, Mirza Tahir wajua,
Nakueleza mwishoni, mauti yaliwafika,
Leo imekamilika, karini ya ukhalifa.

17. Mhariri samahani, naombakuongezea,
Nimtaje mhisani khalifa wetu wa tano,
Masruri Ahmad, Jahazi kashikilia,
Leo imekamilika, karine ya ukhalifa.

Harun R. Bundala,
S.L.P. 54, Tabora.

UKHALIFA KWETU NEEMA

1. Kuukana ni msiba, ukhalifa kwetu neema,
Neema ilo matwilaba, gizani ndiyo najima,
Najima tena ni twiba, pulikani enyi umma,
Ukhalifa kweu neema, kuukana si twayyiba.

2. Kuikana si twayyiba, zawadi yake Karima,
Zawadi 'letayo hiba , hiba kwa wetu Rahima,
Iletayo ukuruba, habithi akawa mwema,
Ukhalifa kwetu neema, yatutenga na ghadhaba

3. Yatulinda na ghadhaba, ilowapata wa nyuma,
Walojitia, ujuba, kuwakana Maasuma,
Salehe hata Shuwaiba, Issa, Musa na Adama
Ukhalifa kwetu neema, ndimo ulimo uzima.

4. Binadamu huwa fisi, ama ageuke kima,
Tenahuwa mufilisi, akaondokwa hekima,
Akamba ana mkosi, akosapo hii neema,
Ukhalifa kwetu neema, ndimo ulimo uzima.

5. Yatuondolea yabisi, ikang'arisha mitima,
Ukaisha wasiwasi, wa kwenda kwenye hutama,
Makao yao waasi, nari yenye kurindima,
Ukhalifa kwetu neema, hidaya yake Quddusi.

6. Sisi tutakuwa sisi, neema tukiiandama,
Tutang'ara ja fususi, daima dumu dawama,
Naima firdausi, 'takuwa yetu makama,
Ukhalifa kwetu neema, ambata ewe insi,

7. Acheni ukaramsi, ushupavu siyo mwema,
Ni kundi la Ibilisi, lisilo na mwisho mwema,
Huyahandisi maasi, kuwaudhi walo wema,
Ukhalifa kweu neema, chonde chonde msiasi.

8. Hawanayo kumbukumbu, mashehe wasio soma
Huonyesha umbumbumbu, wakanapo hii neema,
Ndiyo wachujao m'mbu, ndovu akapita wima,
Ukhalifa kwetu neema, ndiyo wetu utibabu.

9. Sasa nichimbuwe chimbu, mjue msio soma,
Namanga hadi Nanyumbu, sikiza ninayo sema,
Msifuate mkumbu, fanya mambo kwa kupima
Ukhalifa kwetu neema, ni kitaba Maktubu.

10. Twasoma kwenye kitabu, kilichojaa hikima,
Tanzilu yake Wahabu, swiratwa muustaqima,
Sura 'nuru' yahutubu, kwendelea kwa naama,
Ukhalifa kwetu neema, ni kitaba Maktubu.

11. Kunjua ukiratibu, Qadifulaha kisoma,
Juzuu kwenye kitabu, Qara' ya saba tizama,
Aya imestahabu, ahadi yake Hakima,
Ukhalifa kwetu neema, tangazeni wahutubu.

12. Nazidi wapa sahifu, msome mnaosoma,
Asaa mkasadifu, uwaishe uyatima,
Wa kukosa Ashirafu, kiongozi alo mwema,
Ukhalifa kwetu neema, habili yake Raufu.

Mwalimu Majid A. Sudi, (Simba Dume),
Blantyre, Malawi.

IMETIMIA HABARI

1. Chambilecho kimetimu, na leo ni zamu yangu
Awali yangu ni humu, kumuomba Mola wangu,
Anizidishe elimu, niwape pia wenzangu,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

2. Naileza kaumu, hasa nyiye ndugu zangu,
Ametuwekea humu, viongozi kwa mafungu,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

3. Tunapashana elimu, kibawabu ya kingu,
Ndiyo mana tatwehemu, maisha ya kivavangu
Kila kona Islamu, imebakia msungu,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

4. Ni heri yake mjinga, asojua ya maani,
Na mkaja akafunga, kuutafuta undani,
Mola wake atapanga, kumpatia yakini,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

5. Lakini mbanga kupinga, hasa tadi ya moyoni,
Akili ukabananga, ukweli usitamani,
Ni kweli haina kinga, ya kuingia motoni,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

6. Abadi si wa kuvinga, kuwambia ya moyoni,
Ambayo tumeyapanga, kutangaza duniani,
Hususani kwenye tunga, na mengine redioni,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

7. Hii ni yetu sururi, ukhalifa kubaini,
Tumekuwa mashuhuri, kila pembe duniani,
Hivi sasa Masuri, atuongza njiani,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

8. Korombwe darimadari, kimako kwenu cha nini
Mia moja ni dahari, kwa maisha duniani,
Ukhalifa umediri, leo tuu furahani,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

9. Hii kwetu sighururi, njia hasa ya amani,
Tunaishi kwa fahari, twa ongozwa na rubani,
Ukhalifa ni hanjari, ya maovu dunaini,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

10 Hamadia ni jabari, aloliweka Manani,
Kote ni ashahari, kueneza ya Manani,
Mia moja imejiri, hakuna chetu kifani,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

11. Imetimia habari, Mola wetu Mhisani,
Uhalifa utajiri, zama hizi za mwishoni,
Wa utume najadiri, na siyo kiafukani,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

12. Hivi nani muerevu, alopita duniani,
Ajitangaze kwa nguvu, asotumwa na Manani,
Kisha aipate nguvu, ienee duniani,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

13. Aghalabu mpumbavu, atajaribu kuburi,
Atajitutumua mbavu, ili watu wamwamini,
Lakini kwa waelevu, tuna mtupa kapuni,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

14. Ahamadia ni shavu, wanalonga mtaani,
Tuna zitafuna mbavu, leo tupo furahani,
Mia moja ni angavu, leo tupo furahani,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

15. Enyi watu wa dunia, funguweni masikio,
Imetimu ile mia, na miaka ya ujio,
Uhalifa wa dunia, leo ndiyo kimbilio,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

16. Na yule anazonia, tunayo sema si ndiyo,
Basi na aje kwania, atazame shagilio,
Mia moja yatimia, hilo kwetu ni salio,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

17. Karibuni uwanjani, wala mispigwe kicho,
Tuwe wote furahani, msitamani ukocho,
Sisi siyo wazamani, tuwambiacho ni hicho,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

18. Ewe Mola Rahamani, utuepushe na sicho,
Tufurahi kwa amani, shereha bila kificho,
Tuwafunze duniani, waondokwe na kijicho,
Imetimia habari, leo sisi furahani.

Haji H. Mbanga, (Mvumilika)
Ikwiriri, Rufiji.

HADHRAT MIRZA NASIR AHMAD KHALIFATUL MASIH III R.A.

**(Imeandikwa na Chaudhry Muhammad Ali M.A)
na Kufasiriwa na Seif Hassan Nakuchima**

Bwana wetu Mtukufu na Imamu, Marehemu Khalifa wa tatu wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) amewekwa katika mapumziko yake ya kiroho katika ufalme wa Muumba na Mola wake, Ambaye pia ni Muumba na Mola wetu sote. Jamaat ilitingishika kwa khofu ya kifo chake cha ghafla na ilikuwa kama merikebu/boti isiyo na rada katika bahari kubwa ama ni kama mkiwa/yatima aliyeachwa peke yake katika ulimwengu na mazingira magumu kuishi. Ingawa hicho kinaweza kisiwe kipimo halisi cha kiwango cha majonzi tuliyokuwa nayo wakati wa kufariki kwake. Ni kweli tuliachwa yatima lakini hatukuwa peke yetu na kwa hali hiyo hatukuwa kwenye merikebu isiyo na rada. Labda tulinywea lakini si nje ya Mwenyezi Mungu. Tulikuwa na Mwenyezi Mungu Aliye hai, mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu Mola wa Islam Aliyesimama upande wetu na miongoni mwetu na bado alituongoza katika mambo yote (ambayo ni ya kihistoria) baada ya tukio hili la kufiwa. Alikuwa ni tegemeo, kimbilio na shibe yetu. Hata hivyo ni lazima ifahamike ya kwamba saa hizi zilizo baina ya msiba na udhihirisho wa pili wa ishara za kimbingu (Qudrat -e- Thamia) ni saa zinazotia mashaka na khofu kubwa sana. Tuliogopa ila tulikuwa na matumaini sana. Ilikuwa ni hali yenye kujenga fikra na picha. Tulifahamu ya kwamba Mwenyezi Mungu Ametuahidi kutujaalia Khalifa aliyemchagua yeye mwenyewe ikiwa tu Jamaat imefikia kiwango fulani cha kiroho katika uono wake.

Bado kwa kweli ni kipindi cha majaribio na mtihani kwetu wote. Bado pia ilikuwa ni kwa rehema na msaada wake Allah kwamba Alikuwa nasi kwa mara nyingine na Akatujaalia kupitia uchaguzi wake, Khalifa Aliyemchagua yeye Mwenyewe, udhihirisho wa nne wa Matakwa yake, mrithi mwenye kufaa wa Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi (a.s), Hadhrat Sahibzada Mirza Tahir Ahmad, Mwenyezi Mungu Ampe umri mrefu, Afya njema, uimara na mafanikio katika kila jambo lake na kwamba Mwenyezi Mungu Atujaalie ujasiri na kiwango kizuri cha kumfuata kwa kadiri ya uwezo wetu. Kuchaguliwa kwake kufikia katika kilele hiki na kuwekwa kwenye cheo hiki kikubwa ilikuwa pia ni mafunzo ya aina yake ya kiroho. Yalikuwa ni mafunzo ya haki tena ya kina mno yenye kutetemesha moyo na roho kwa mtu binafsi na wote kwa pamoja ambayo Jamaat iliibuka imeimarika, yenye uhakika na iliyoundwa vizuri zaidi kuliko ilivyokuwa kabla.

Wasiwasi wetu ulipotea kama ndoto na badala yake tulijawa shukrani na faraja kubwa sana. Jamaat ilijikuta mara ya nne ya kurithiana baada ya kufariki kwa Mwanzilishi wake Mtukufu.

Hivyo kusonga mbele kwa jeshi hili la kiroho la kiislam kunaendelea kwa hamu na nguvu mpya tena iliyokubwa. Tuna furaha na tunatoa shukrani kubwa kwa Mwenyezi Mungu hakutuacha katika saa na wakati ule tuliohitaji msaada wake, tuna huzuni pia. Tuna mawazo yaliyokutana kwa kupotelewa na kufanikiwa kushinda khofu na kupata furaha na matumaini. Ni mafunzo yenye maana sana tena yanawezekana tu katika kiwango cha imani ya kweli ya kiroho.

Muda wote huu wa matatizo kwa kweli inaonekana ni mwendelezo na upanuzi wa yale yaliyopita kuyaleta katika hali mpya, ukiachia mbali mambo madogomadogo yaliyojitokeza. Aya za Qur'an Tukufu bila ubishi zimekuwa zikitueleza ya kwamba mashaheed yaani mitume, makhalifa na wale waliouawa kwa njia ya Allah, hawafi bado wako hai. Wanaishi kadri mambo yao walioanzisha, madhumuni na mafanikio ya yale waliyoanzisha yanaendelea kupatikana pamoja na ukweli kwamba warithi na wafuasi - wao wanaendelea kuishi na kutekeleza kwa dhati madhumuni haya. Hadhrat Hafidh Mirza Nasri Ahmad, Marehemu Imamu wetu hajafa. Kwa hiyo siandiki maelezo haya machache kulalama na kuelezea kifo chake, la khasha; ila ninaandika kumkumbuka kwa namna ninavyomuona yu hai katika moyo na akili yangu. Pia madhumuni ya makala hii si kuelezea historia nzima ya maisha yake, kwa sababu kufanya hivyo itakuwa ni kazi nzito sana. Kwa mtu mnyonge tena mwenye upungufu mwingi kama mimi. Kwa hiyo nitajikita tu katika yale ambayo watu mbalimbali wameweza kuyashuhudia. Nitajitahidi pia kuelezea yale niliyo yaona binafsi na katika baadhi ya Maeneo machache tu nitaelezea yale ambayo Watu wengine pia waliyaona bila ya kufuata mtiririko wa matukio yenyewe. Kwa kweli ninajiona kama nguchiro ambaye natakiwa kuelezea mlima mkubwa kwa maana ya Huzur, maana marehemu Imamu wetu alikuwa ni mkubwa zaidi ya milima mikubwa sana. Alikuwa ni zawadi na muujiza wa Mwenyezi Mungu Aliyotuletea sisi na binadamu wote kwa ujumla. Mwenyezi Mungu kwa elimu yake kuu na Hekima alijua aina ya kiongozi aliyetufaa sawa na wakati ule. Alikuja hasa kwa wakati uliofaa. Muda na nafasi hautoshi kueleza undani wa yeye alivyo na yale mengi aliyoyafanya. Aliishi katika nyakati zenye misukosuko na hivyo ndivyo ilivyokuwa hata kwa Jamaat. Namna alivyokabiliana na changamoto zilizokutana naJumuiyya na kuzishinda katika hali ya Uimara na kuiokoa Jamaat ni suala linalotia moyo sana, busara ya hali ya juu na uvumilivu, kifua kipana na utegemezi wa kipekee kabisa kwa mmoja tu aliye ni chemchemi ya msaada na mwongozo ambaye ni Allah, pia inaimarisha imani yetu kwa wakati huu na ujao kwa sababu wote tumeshuhudia na kuhakikisha zaidi kwamba Imamu na khalifa wa zama amechaguliwa kutoka mbinguni na kukirimiwa uwezo mkubwa wa kuingoza Jumuiyya katika hali yoyote itakayojitokeza mbeleni.



***Hadhrat Mirza Nasir Ahmad
Hadhrat Khalifatul Masih III
r.h.a***

Sasa tukirudi kwenye somo letu, tuanze mwanzo kabisa. Nionavyo mimi sehemu ya Maisha ya Huzur kabla ya ukhalifa ni muhimu sana. Katika Qur'an Tukufu Mwenyezi Mungu Amefanya Mtume (s.a.w) aeleze hivi; "Nimeishi kati yenu maisha yangu yote, Je hamkumbuki?" Mtume (s.a.w) aliishi kwa miaka arobaini na watu wa Makka na walimfahamu vema kwamba alikuwa ni mtu mkubwa wa aina yake. Wangeweza kupima vitendo vyake vya sasa kwa kuangalia yaliyopita. Hii pia ni kawaida katika tafiti za sayansi kwamba tunaanzia tunakojua kuelekea tusikojua, kutoka kwenye yanayoonekana kuelekea kwenye yale yasiyoonekana. Imani juu ya yasiyoonekana inategemea mwamba ugumu wa yale yaliyoonekana, yaliyochunguzwa na pia yale ambayo watu wamezoea kuyaona kwa hiyo ukweli wa Mtume Mtukufu (s.a.w) sio ila ni nakala ya ukweli wa mwanawe wa kiroho Masihi Aliyeahidiwa (a.s) na warithi wake (yaani Makhalifa). Kwa maana hii kuangalia maisha ya Huzur kabla ya kuchaguliwa kama Khalifa ni jambo lenye maana na malipo makubwa sana.

Maisha ya Huzur kabla ya ukhalifa ni kitabu. Mwandishi alikuwa na heshima ya kumchunguza kwa karibu sana khalifa tangu walipokuwa karibu naye sana mwaka 1944. Kuhusiana na maisha yake kabla ya mwaka 1944, nitawanukuu wengine; Mirza Muzaffar Ahmad, Mirza Zafar Ahmad, Mirza Dawood Ahmad aliye ni binamu yake na mchezi mwenziwe katika siku za awali za utoto wao.

Hadhrat Amman Jan, mke Mtukufu wa Masihi aliyeahidiwa (a.s) na bibi wa Huzur alimfanya Huzur kuwa mwanae binafsi na alimfanya kutoka nyumba ya wazazi wake kwenda kwenye makazi ya Hadhrat Amman Jan. Mirza Muzaffar Ahmad anaelezea; kabla sijajiunga na chuo huko Lahore, baba yangu alinipeleka pia kwa Hadhrat Amman Jan hivyo Huzur nami tulishi pamoja tena wenye furaha. Niligundua ya kwamba Huzur aliomba ruhusa kila alipotaka kuondoka kwenda kokote. Maneno ambayo Hadhrat Amman Jan aliyatumia kumruhusu bado yanagonga kichwani kwangu; alikuwa akisema "ndiyo mpendwa unaweza kwenda. Mwenyezi Mungu Awe kimbilio na nguvu yako". Alikuwa akitamka maneno haya akiwa - amejawa na mapenzi na mategemeo ya hali ya juu sana, kadiri ninavyokumbuka mambo ya zamani ninamuona Huzur ameketi ndani ya Masjid Mubarak akisoma masomo yake ya Qur'an Tukufu kutoka kwa Hafiz Muhammad Ibrahim, akighani na kurudia rudia ili kuifanya inate kwenye kumbukumbu, kwa sababu mafunzo yake ya mwanzo na ya msingi ilikuwa ni kuhifadhi Qur'an Tukufu. Tulikuwa tunakula chakula chetu cha mchana na Hadhrat Amman Jan. Mara nyingi yeye mwenyewe Hadhrat Amman Jan alikuwa akiandaa chakula na kutugawia chapati za moto.

Wakati wa baridi chakula cha usiku tulikuwa tukila katika chumba kikubwa ambacho kilikuwa ni chumba chetu cha kulala ambacho pia ilikuwa unapita ili kufika Baitul - dua, chumba kidogo cha kuswalia. Chakula kilikuwa kikiandaliwa aidha kwenye mkeka au kwenye meza ndogo fupi ambayo tungeweza kukaa. Wakati wa baridi, chakula cha jioni kilikuwa kinaliwa sehemu ya juu ya nyumba ambako pia kilikuwa kikiwekwa kwenye aina fulani ya meza ya mbao.

Hadhrat Musleh Mauud (r.a) alikuwa akimtembelea Hadhrat Amman Jan, mama yake kila siku mara tu baada ya sala ya Maghribi na alikuwa akikaa naye kwa muda mrefu. Alikuwa akitembea kwenye chumba au kuizunguka nyumba wakati akiongea na Hadhrat Amman Jan. Nyakati hizi baba yangu Mirza Bashir Ahmad (r.a) alikuwa pia akiungana nao. Wakati wa likizo, Hadhrat Mamoon Jan, Dr. Mir Muhammad Ismail (kaka wa Hadhrat Amman Jan) pia walikuwepo. Mazungumzo yalihusu zaidi mambo ya dini kama vile Ahmadiyyat na Islam. Chakula cha jioni tulikuwa mara nyingi tukila baina ya sala ya maghribi na Insha na kilikuwa kikitolewa baada ya kuondoka kwa Hadhrat Muslih Mauud. Nakumbuka Muslih Mauud wakati wa moja ya matembezi yake akituhutubia watoto alisema; "Qur'an Tukufu ni neno la Mwenyezi Mungu. Ni chemchem ya maarifa. Tengenezeni tabia ya kuizamia na kuifikiria sana". Ikiwa hutapata kitu cha thamani lakini utaishia kupata ganda lake kuonyesha ya kwamba kuzamia ndani ya bahari hii ni tabia yako". Siku hizo kwa kweli zilikuwa ni za mapenzi na furaha. Ilikuwa ni katika aina hii ya mazingira mazuri yenye kila namna ya ukweli ambayo Huzur alikulia chini ya huruma, mapenzi na usimamizi binafsi wa Hadhrat Amman Jan. Baada ya kuhifadhi Qur'an Tukufu, Huzur alifaulu mitihani yake ya kiarabu kwa kiwango cha juu kabisa (Honours in Arabic) kutoka chuo kikuu cha Punjab na baadae alijiunga na chuo cha serikali mjini Lahore ambako alisoma kwa muda wa miaka minne na alifaulu katika mitihani ya shahada ya kwanza ya sanaa. Katika siku hizo bweni la Ahmadiyya lilikuwa barabara ya Sinagogi (Temple Road) na baadae lilihamishiwa Chauburji, katika barabara ya Bahawalpur. Katika kukaa kwake Huzur alianzisha mlolongo wa kutengeneza vijarida vidogo vilivyochapishwa kwenye karatasi nzuri sana na kusomeka kwa dakika chache sana. Uchapishaji na usambazaji wake ulileta mvuto sana katika maisha ya chuo na ilithibitika kuwa ni njia yenye manufaa katika kuwasilisha ukweli. Hii ilisababisha midahalo na majadiliano katika vikundi vidogo vidogo ambavyo vilihusisha wanafunzi Waahmadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya.

Kuhusiana na vijarida hivi Daktari A.R Tabassum mmoja wa wanafunzi wenziwe Huzur na mshindi wa zawadi ya Rais kutokana na kitabu chake cha Maneno ya Hekima kwa mashariki (wisdom to the East) anatoa maelezo mazuri yafuatayo:-

"Kama wiki mbili hivi baada ya chuo kufunguliwa kutoka likizo fupi Huzur alianzisha chama kilichoitwa kumi bora (The top ten) ambacho kwa kura nyingi Huzur alichaguliwa kuwa Rais wake. Iliamuliwa ya kwamba

Itaendelea Toleo lijalo, Inshaallah.

HADHRAT MIRZA TAHIR AHMAD KHALIFATUL MASIH IV

Na Sheikh Ahmad Daud
Mmoto, Morogoro

Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale waliamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa kama wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabidilishia amani badala ya hofu yao. Wataniabudu, wala hawatanishirikisha na chaochote. Na atayekufuru baada ya haya basi hao ndiyo wavunjao amri." (24:56).

Mwenyezi Mungu katika aya hii ameeleza faidi tatu za uongozi wa Ukhalifa.Kuimarika kwa dini, kubadilika kwa hofu katika amani na waaminio kupata nafsi ya kufanya ibada yake kwa utulivu na amani.

Katika makala haya pamoja na kufahamu maisha ya Hadhrat Khalifatul Masih IV, Mirza Tahir Ahmad tutashuhudia pia ni kwa jinsi gani faida hizi tatu zimepatikana katika uongozi wake wa ukhalifa.

Lakini kabla hatujataza-

jisikia furaha kubwa kuandika makala hii yanayohusu maisha yake. Ninaona furaha kwa sababu mtu ninayemuandika ni mtu ninayemfahamu kwa kuwa muda wangu mwingi nikiwa masomoni Rabwah Pakistan katika Chuo cha Wabashiri wa Jumiya ya Waislamu Waahmadiyya nilihusika naye katika shughuli nyingi. Hivyo ni mtu ninayemfahamu.

Hata hiyo furaha hii inaingiwa na doa, kwa sababu yule tuliyemzoea kwa jina la Mirza Tahir Ahmad hayupo tena duniani - amefariki. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Kadri fikra zinavyoingiza katika bahari ya kumbukumbu yake ndivyo moyo unapoingia katika kilindi cha simanzi na huzuni. Hii kwa sababu macho hayamuoni tena.

KUZALIWA KWAKE

Mirza Tahir Ahmad ni mtoto wa Hadhrat Mirza Bashiru- Din Mahmood Ahmad r.a., Khalifa wa Pili. Mama yake ni Bi Mariam Siddiqah aliyekuwa mke wa tatu wa Khalifa wa Pili. Mirza Tahir Ahmad alizaliwa tarehe 18, Desemba, 1922 mjni Qadian.

Tayari nyuma yake mama yake alikwisha zaa dada zake wawili. Bi Amatul Hakim na Amatul Basit. Baadaye alizaliwa mtoto wa kiume ambaye kama angekuwa hai angekuwa kaka kwa Tahir. Lakini alifariki katika umri mdogo.

Kuzaliwa kwake kuliambatana na viashiria vya sifa zake.Kipinidi hiki kilishuhudia sehemu ya Qadian mieleka ya kijadi (kabadi kwa lugha ya Kipanjabi). Mtu hutumia sana afya, ujana na kasi ya mbio. Baada ya kumgusa mmoja na wachezaji wa timu pinzani ambayo huwa wanajipanga upande mmoja na timu yake upande mwingine, mchezaji hurudi kundini kwa huyu akiwakwepa wapinzani wake wasimshike, kwa kasi. Kama inatokea kukamatwa hutumia afya yake ili kijinasua kutoka kwa maadui.

Katika mechi moja inayosemekana Tahir alipomkamata mpinzani wake alimtengua nyonga, tukio hili lilidhihirisha afya yake kama kijana. Baba yake Khalifa wa Pili r.a. alipopata taarifa alimpiga marufuku kucheza kabadoli. Hata hivyo aliendelea na michezo mingine kama kukimbia.

Nakumbuka nikiwa chuoni nilikuwa miongoni mwa wacheza mpira wa meza wazuri. Khuddam Ahmadiyya iliandaa mashindano yake. Baada ya kuruka ngazi nilitinga fainali. Mpinzani wangu katika mechi ya fainali alikuwa kijana Ridhwan Ahmad. Alikuwa mrefu zaidi yangu mwenye kutumia mkono wa

kushoto. Mwisho mimi nilikuwa mshindi. Mgeni rasmi aliyegawa zawadi alikuwa Mirza Tahir Ahmad ambaye mbali na vyeo vingine pia alikuwa mlezi wa wanafunzi wa kigeni katika chuo chetu cha Wabashiri. Baada ya kugawa zawadi aliniambia: *Dayddy come let us have a match. I wanto to assess my playing ability with the champion*." yaani Daddy njoo tucheze mechi, nataka kutathmini uwezo wangu wa mchezo kwa kucheza na bingwa." Akaingia chumba cha kubadilishia nguo, akavaa trach suit nikacheza naye. Nilimshinda kwa taabu, ingawa alicheza bila ya mazoezi. Tukio hili pamoja na kuonyesha jinsi alivyopenda michezo, lakini pia linadhihirisha jinsi alivyokuwa mtu mwenye kujichanganya na watu kiasi kwamba unapokokuwa naye pamoja haonyeshi ukubwa alionao kwake.

Mirza Tahir alilelewa vizuri sana. Ingawa alikuwa mtoto wa pekee wa kiume katika nyumba, lakini hakudekezwa na wazazi wake. Walihakikisha anasoma masomo yote ya dini na hasa Kur'an. Mama yake alipata sifa ya pekee ya upendo kwa wengine.

Ndiyo maana kama kuna mafundisho aliyomwachia Tahir yalikuwa dini ya upendo. Sifa hii ya upendo wa ajabu tutaishuhudia huko mbele pia, wakati akiwa mtu mzima.

Mbali ya hayo, Tahir alikuwa na sifa ya kuwa na ucheshi. Ndugu zake walipokuwa wamefanya makosa, walimchaguwa yeye kusema mbele ya baba yao. Hawakufanya hivyo kwa kuwa alikuwa na uwezo wa kujieleza kuliko wao, bali kwa sababa



Hadhrat Mirza Tahir Ahmad Hadhrat Khalifatul Masih IV r.h.a.

ya ucheshi wake. Alizungumza na baba yao kuhusu makosa yao kwa namna kwamba baba badala ya kukasirika aliishia kucheka.

Watoto wengine wahakujaaliwa sifa hii ya ucheshi wenye busara. Nakumbuka tukiwa wadogo tulikuwa tunasoma chuoni, mwalimu baada ya kufanya mapitio ya masomo ya jana yake aligunuda hatukuwa tumeyapitia na kuyakumbuka.

Alituamuru kwenda kukata viboko. Sote tulileta ila Hassani. Baada ya kungoja kwa muda mrefu alituambia kumtafuta. Tukaenda tusimuone. Punde akaibuka kutoka katika chumba kilichokuwa karibu na pale tulipokuwa tunasoma na mchi mkononi. Mwalimu alimuuliza, " Hii ndiyo fimbo?" Kijana Hassani akajibu: Ndiyo hii ndiyo fimbo inayofaa, maana kila siku unatupiga viboko." Mwalimu aliishia kucheka. Kuanzia hapo hatukuadhibiwa tena.

Akawa anatuokoa. Ndiyo aliyovyokuwa Mirza Tahir. Aliyatatua na kusawazisha hitilafu baina yao na baba yao kwa ucheshi wenye busara kiasi kwamba baba yao alibaki anacheka kwa furaha.

MASOMO YAKE

Masomo yanayofundishwa kwa shuleni huwa yameteuliwa na kupangwa rasmi (sylabus) ambayo mwanafunzi anahitajika kusoma vitabu vyake vya kiada ili kufaulu katika mtihani. Lakini toka mwanzo wa masomo yake Mirza Tahir hakuwa na utaratibu wa kusoma vitabu hivyo vya kiada tu bali alikuwa amejenga mapenzi ya kusoma vitabu vingine katika somo husika na hivyo kupanua ufahamu wake.

Mwaka 1944 alifaulu mtihani wake wa Matriculation ambapo kwahapa kwetu nchini mtihani huo ni sawa na C.S.E.E. (Certificate for Secondary Education Examination). Pia ni mwaka alipofariki mama yake Bi Mariam Sidiqah. Ingawa kifo hicho kilisababisha simanzi kubwa sikuacha kujisomea. Muda ni kipindi ambapo alifanikiwa kusoma fasihi za Kiurdu na tafsiri za fasihi za Kiingereza kama Shakespear, Charles Dikens, Canan Doyle na waandishi wengine wengi.

Wazazi wake walipendelea Tahir awe Hafidh wa Kurani. Akiwa katika jitihada hizi alijikuta anajenga mapenzi ya tafakari ya falsafa na hekima yake zaidi katika kuhifadhi matini yake. Sambamba na usomaji wa Kurani kwa kuwa alikuwa anasoma vitabu vya fasihi na sayansi alijenga tabia ya udadishi juu ya mambo aliyoyasoma. Ni wakati pia alipogundua maktaba ya baba yake. Humo alikutana na vitabu vya kisayansi vinavyozungumzia nadharia ya Darwin na wataalamu wengine wa elimu ya sayansi juu ya jinsi dunia ilivyoumbwa. Wakati huu alikuwa kijana wa miaka 14.

Umri wake mdogo haukumfanya aelewe sawasawa mambo haya. Hata hivyo vitabu hivyo vilimpa mwamko na fikra. Akaanza kuhoji, Mungu yupo? Katika harakati za kutafuta jawabu la swali hili, bidii za kujisomea zilizidi kiasi kwamba alijikuta wakati mwingine usingizi umempitia na kitabu mkononi. Huenda kipindi hiki cha zoezi hili ndipo

ugonjwa ulipomsumbua kwa muda mrefu wa maumivu makali ya kichwa (nugraine) uliompata.

Hapo kabla hakuwa na shaka yoyote juu ya ukweli wa mafundisho ya dini ya Kiislam kwa mtizamo wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Kilichokuwa kinachomkera zaidi ni kwamba mafundisho hayo yalitoka kwa Mungu kweli aliye hai? Kama jawabu la swali hili ni hapana, basi mafundisho hayo ya dini yanabaki kuwa mazingamgu ya kitaalamu yaliyokusudiwa kuchangamsha tu akili za watu lakini hayana maana nyingine yoyote.

Tahir akaanza zoezi la kumwomba Mungu kwa njia ya dua na sala. Mwenyewe anasema "Huu ulikuwa ni muda mgumu sana kwangu. Sikuwa na wasiwasi kwamba kinadharia ni kweli Mungu yupo. Lakini nitapataje yakini?, je anaweza kujidhihirisha kwangu?".

Maswali haya yalimfanya awe na udadisi mkubwa. Yalimfanya adumu akisali msikitini na muda mwingine nyumbani. Aliomba "Ee MwenyeziMungu Mola wangu kama kweli wewe upo basi jidhihirishe. Mimi ninakutafuta, nionyeshe ulivyo waila nikipotea wewe utawajibika halitakuwa kosa langu, siku moja alijikuta akiwa katika hali ya kuwa na bumbuwazi. Akaona Kashfi ambapo dunia ilionekana imesinyaa mithili ya mpira mdogo. Kila kitu kilicho hai juu yake kilikuwa kinatingishika kwa pamoja kilitoa sauti Mungu wetu ni Mungu mmoja na kukariri sababu ya kuwepo kwao duniani na kuanza kumtukuza yeye. Mara nilishuudia mwanga umetapakaa sehemu zote. Kila kitu kilichokuwa juu yake kiliimba na kusinyaa kwa pamoja kama unavyofanya mwili wa binadamu anapopumua. Nilijikuta na mimi nikitamka maneno yale yaliyotamkwa navyo, Mungu wetu ni Mungu mmoja hata nilipoamka na kuwa katika fahamu zangu niliendelea kutamka maneno

haya na kuendelea kuyashuhudia maajabu haya. Kuanzia hapo sikuwa na shaka tena juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu". Mirza Tahir alisema "kipindi kingine cha masomo ni pale alipofuatana na baba yake alipokwenda kutibiwa jeraha lake shingoni baada ya kushambuliwa na Sunni mmoja. Baada ya jitihada kubwa tiba yake ilishindikana kupatikana kule Pakistani. Akashauriwa kwenda Uingereza. Baada ya matibabu baba yake aliamuwa kumwacha Tahir London kwa ajili ya masomo kwa msaada wa Sir RalphTurner alijiunga na chuo kikuu cha London cha tamaduni za nchi za Mashariki na mila za Afrika. Pale alisoma sarufi na lafidhi safi (phonetics) ya Lugha ya kingereza pamoja na hayo alipata nafasi ya kufahamu tamaduni za watu wa nchi za Mashariki na maisha ya Waafrika ili kupata elimu zaidi juu ya tabia za watu wengine. Tahir alitumia muda wake pia kusafiri katika nchi za Ulaya na Amerika. Fursa hii ilimpa elimu zaidi ya kufahamu tamaduni za Wazungu katika nchi zao mbalimbali. Kwa ujumla, hii ilikuwa fursa yake kubwa ya kufahamu mambo ya kijamii katika sehemu mbalimbali za dunia na kupanuka kifkra, Mungu alikuwa anafanya maandalizi ambayo yangemsaidia baadaye kama kiongozi wa watu wa jamii mbalimbali za dunia, kwa kuwa kwake Khalifa.

Aligundua kuwa katika kuhoji mambo haya alikuwa anautikisa msingi mzima wa kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Alichotaka hasa ni kumjua Mwenyezi Mungu lakini si kwa njia ya kusoma vitabu tena bali kwa njia ya utambuzi wa moja kwa moja. Akaanza na kuyachambua mambo hayo kwa kutumia mantiki. Akagundua kwamba kuna utengano wa aina fulani uliopo baina ya vitu. Kwa mfano mtu anatambua kuna wadudu wapo. Lakini kwa upande wa pili wadudu hawatambui kuwa kuna binadamu. Ni kwa jinsi hii Mungu anafahamu kuwa mwanadamu yupo. Lakini mwanadamu hafahamu kuwa Mungu yupo. Hivyo kama utengano upo baina ya wadudu na mwanadamu basi utengano upo baina ya mwanadamu na Mungu.

Endelea Uk. 10

HADHRAT MIRZA TAHIR

Kutoka Uk. 9

KHULKA ZAKE NJEMA

Baada ya kufariki mama yake Tahir alilelewa na mam**a** zake wadogo. Kwa hali hii alipata fursa ya kupata Sunna ya Mtume Muhammad s.a.w ya kufiwa na mama yake katika umri mdogo.

Kwa ujumla Mirza Tahir kwa kulelewa na mama zake wawili wadogo na kuzungukwa na dada zake alipata mapenzi makubwa. Pia mazingira haya ya upendo yalimuathiri hata yeye katika maisha yake ya baadae. Kwani mazingira ya akina mama yana upendo zaidi kuliko yale ya akina baba. Ndio maana katika khulka njema alizokuwa nazo, upendo uliongoza. Aliguswa sana alipoona maonevu yakifanywa kwa wanyonge, naye hakusita kuwasaidia.

Katika safari yetu Pakstani tukiwa katika refresher course tulipata fursa ya kutembelea makao makuu ya ofisi ya Waqfu-e-Jadid. Tulipata fursa ya kuonana na mkurugenzi wake. Tulimuuliza yeye amerithi nafasi ile kutoka kwa Mirza Tahir Ahmad, je ni jambo lipi alilojifunza kwake?, jawabu lilikuwa katika neno moja tu, Upendo. Siku moja alitembelewa na mwalimu mmoja aliyekuwa anafanya kazi ya malezi kwenye jamat moja iliyopo katika jimbo la Sidhi ambalo hali ya maisha ni duni. Posho aliyokuwa anaipata haikuwa inatosha kumudu maisha, hivyo alikuwa amekuja kwake kuacha kazi. Alipofika tu ofisini kwake alimpokea kwa maneno matamu. Akapewa kiti na kinywaji baridi, alipoeleza nia ya kuja kwake, hakumjibu. Alivua koti alilokuwa amevaa siku ile akamvalisha yeye, akampa fedha mara mbili ya posho yake na kumwambia kuanzia sasa hii ndiyo itakayokuwa posho yako, mwalimu alidondosha machozi kwa furaha na kuathirika na mapenzi aliyopata. Aliondoka na kurudi kazini akiwa na ahadi ya kutoacha kazi hii mpaka mauti yamfikie.

Ninakumbuka mwaka 1982 alipochaguliwa kuwa Khalifa, Khalifa wa tatu Hadhrat Mirza Nasir Ahmad (r.a) rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake aliwapangia posho maalum wanafunzi wa kigeni waliokuwa wanasoma katika chuo cha wabashiri Rabwah. Posho hii ilikuwa kwa ajili ya likizo wakati wa msimu wa joto. Ambapo wanafunzi walikuwa wanaenda kupumzika kwenye sehemu zenye hali mzuri ya hewa, kama **Muree,** Kashmir au Queta. Mwaka ule ilikuwa imechelewa kutolewa. Mimi nilikuwa rais wao (President for Foreign Students Union). Nilimwandikia mkurugenzi wa elimu bwana Nasir Seif kwa wakati ule atume posho hiyo kwani hali ya joto ilikuwa inazidi na wanafunzi walikuwa wameshaanza kuathirika kwa kupata majipu na tete kuwanga. Asijibu nami nikaandika barua ya pili ya kukumbushia, pia asijibu.

Mirza Tahir Ahmad alikuwa mlezi wetu kabla hajachaguliwa kuwa Khalifa. Akatuita kwenda kuonana naye. Baada ya mazungumzo mengi kama baba na watoto tuligusia barua yetu kama aliipata iliyohusu kuchelewa kwa posho na kuathirika kwa wanafunzi kulikotokana na joto. Akajibu hajaipata. Alibadilika rangi mara moja kwa hasira, na kuwa mwekundu zaidi. Akaitwa bwana Seif na kuamriwa kuandaa mara moja yale yote yanayohitajika kwa ajili ya safari yetu.

Kutoka siku ile aliteremshwa cheo. Na hakufanya haya ila ni kwasababu ya kuguswa na hali zetu za unyonge.Wakati fulani tulikwenda Lahore kupumzika wakati wa likizo ya mwisho wa juma. Tulipewa malazi katika sehemu ya juu ya jumba la wageni katika Jamaat ya Lahore. Siku ya pili tulipokuwa tunateremka kwenda matembezini tulielezwa kuwa Patron wetu alikuwa amewasili jana yake pamoja na familia yake. Nilipowauliza kwa nini wasituarifu tukateremka na kumpisha yeye? Walijibu, aliambiwa juu ya kuwepo kwetu. Akawaambia wamtandikie magodoro chini panatosha. Yeye alikuja kikazi na sisi tulikuwa Lahore kwa ajili ya mapumziko. Huyu ndiye Mirza Tahir mtu ambaye hakuwa na makuu. Mnyonge kwa wanyonge lakini mkali kwa mafedhuli wenye hali. Ni muhali kwa zama hizi kupata kizazi cha aina yake. Watu ambao raha kwao sio raha yao bali ni raha ya wenzao.

MAJUKUMU YAKE KABLA HAJAWA KHALIFA

Ingawa msimamo wa jamaat Ahmadiyya ni kuwa serikali yoyote inayotoa uhuru wa kuabudu ni serikali njema na kwamba yenyewe haina mtizamo wowote wa kisiasa, hali hiyo inawahimiza wafuasi kuwa karibu na serikali yao ili kujua haki zao ili kupata fursa ya kutoa ushauri mwema ili kupata mafanikio yanayokusudiwa. Kwa ajili ya nia hii njema ya kuishauri serikali kufanya mambo yake vizuri Khalifa Mtukufu wa III r.a alimtaka Mirza Tahir Ahmad kama mshauri wa mambo ya kisiasa kutoka katika jumuiya ya Ahmadiyya kwa ajili ya serikali ya Pakistani. Kipindi hiki waziri mkuu alikuwa bwana Zulfikar Ali Bhutto. Bila ya kutia chumvi, mafanikio makubwa ya kisiasa aliyoyapata Bhutto yalitokana na ushauri wake. Mapema wakati wa maandalizi ya kampeni ya uchaguzi mkuu ilibidi abadili mbinu zake kutokana na wazo lake Tahir. Bhutto alikuwa atumie sera za kijamaa kunadi serikali yake. Mirza Tahir Ahmad alimwambia sera hizo hazifai. Nibora kutangaza sera usawa wa binadamu zilizonadiwa na mtume Muhammad s.a.w, sera hizi zilimfanya ashinde kwa kishindo.Tokea hapo Tahir amekuwa mshauri wake mkubwa wa mambo ya kisera za kisiasa za Bhutto. Lakini baadaye aligundua kuwa Bhutto alikuwa na tamaa ya ukubwa katika nchi zinazojiita za Kiislam, pia alikuwa amezungukwa na wapambe ambao walikuwa maadui wa Jumuiya. Ili kufikia lengo lake ilbidi asikilize na kukubali ushauri wao ukiwemowa kuachana na mahusiano na Jumuiya. Na mwaka 1974 alitangaza kuwa ni Jumuiya ya watu wachache (minority) wasio na haki yoyote ya kiraia sawa na wengine na kwamba wao hawakuwa Waislamu. Baadhi ya wanajamati walimlaumu sana Tahir kwa kuwa kwake mshauri wa mtu ambaye baadaye amekuwa adui mkubwa. Katika moja ya hotuba zake za mwanzoni baada ya kuchaguliwa Khalifa alisikika akisema "Alikuwa anajuta kusaidia mtu mpaka akaingia madarakani, lakini baadaye akabadilika na kuwa adui mkubwa wa Jumuiya na kuteseka katika mkono wake, leo hii mimi nimechaguliwa kuwa mlinzi na mtetezi mkuu wa Jamaat ambayo ilonekana kana kwamba niliisaliti, kwa bahati mbaya mateso haya yanaonekana kusababishwa na mimi kwa kumsaidia Bhotto. Nilifanya hivi kwa nia njema ya kuwasaidia wananchi wapate serikali iliyobora. Nitamuomba Mungu afanye uwamuzi wake juu ya mambo haya". Hazikupata siku nyingi Bhotto alikamatwa na Zia-ul-Haq na kunyongwa. Jukumu jingine alilokuwa nalo ni kuwa mlezi wa wanafunzi wageni katika Jamia Ahmadiyya, chuo kinacho toa mafunzo ya Masheikh au Wabashiri katika Jumuiya ya Ahmadiyya. Jukumu lake hasa lilikuwa kuhakikisha usitawi wao. Moja ya program zilizokuwa zinafanyika kila mwaka, pikiniki iliyokuwa katika shamba lake la bustani nje kidogo ya mji wa Rabwah. Mpango huu ulikuwa unafanyika wakati wa msimu wa Spring (msimu wa hali ya hewa mzuri katika miezi ya March hadi April) jambo la maana la kuzingatiwa katika program si ile furaha za waliokuwa nayo wanafunzi wa kigeni ya kubadilisha mazingira ya masomo na kupata furaha bali jinsi alivyoiandaa kwa namna ya pekee. Wanafunzi wa sehemu mbalimbali za dunia walipewa fedha sawa na mahitaji yao. Wakaambiwa kupika chakula wanachokula katika nchi zao. Pia siku ile tulivaa mavazi yetu ya Kitaifa, vyakula vililiwa pamoja. Tulijikuta kwenye furaha ya ajabu. Jamii yenye watu tofauti ikiwa kwenye meza moja wakila vyakula vinavyoliwa duniani kote. Mkusanyiko huu ulituongezea upendo na umoja, mbali na furaha ya ajabu. Tahir ni kweli alifahamu khulka za watu wa jamii mbalimbali duniani. Ndio maana yeye aliwapenda na wao wakampenda. Kwa neno zima alikuwa ni mtu wa watu.

Mbali na Mkurugenzi wa Waqfe-Jadid aliteuliwa kuwa afisa mkuu wa mkutano wa mwka pale Rabwah, pamoja naye alikuwa wapo Chaudhry Hamidullah. Chini yaofisi yake mimi na Abdul-Ghaffar, kijana tuliye kuwa naye chuoni tukisoma naye. Tulikuwa tunazungukia maeneo yotena kuleta taarifa ya matukio yote mahimu. Abdul Ghaffar kwa sasa ni Mbashiri wa msikiti wa Baitul Futuh mjini London. Yeye ni kujana kutoka Ghana, Afrika ya Magharibi.

Kama kawaida yake ya unyenyevu sisi alitupatia baiskeli mpya. Yeye mwenyewe alikuwa na baiskeli yake ya zamani iliiyokuwa kuu-kuu. Sisi na hata maafisa wenzake walikuwa wanaenda majumbani kwao usiku wa manane kupumzika. Lakini yeye aliendelea kuwepo ofisini akichapa kazi usiku wote na mchana kutwa. Hata kama muda huo ulikuwa usiku wa manane. Mara nyingi Jalsa Salana ilipomalizika Mirza Tahir aliachwa mgonjwa kwa sababu ya kazi ngumu.

MIRZA TAHIR AHMAD AWA KHALIFA

Tarehe 10 June, 1982

Mirza Tahir Ahmad alichaguliwa Khalifa. Katika wajumbe 148, wajumbe 130 walimpigia kura za ndiyo. Wajumbe walitoka katika jamaat za nje na ndani ya Pakistan. Katika hawa walikuwepo wakuu wa ofisi zote za Jamaat Ahmadiyya Rabwah, Sadri Anjuman na Tahrik Jadid Almad, marais na Ma-Amir wa kutoka jamaat za ndani na nje ya Pakistan.

Wajumbe hawa walitoka India, Uingereza Marekani, Canada, Ujerumani, Ufaransa, Udachi, Indonesia, Malasia, Spain, jumuiya za Afrika Magharibi na Afrika Mashariiki.

Ni vizuri ikaeleweka kuwa mchakato wa wachaguzi wa Khalifa haufanani na ule wa kisiasa. Kinachozingatiwa kama roho ya mtu ni mcha Mungu. Anayeshiriki ni lazima awe mcha-Mungu na anayechaguliwa pia. Ucha Mungu ndiyo unaotawala mambo yote. Kura huwa kwa kuinua mikono ili kuwafanya wote wanashiriki kuwa makini kuna kiapo rasmi ambacho kila mmoja ni lazima ale: Kiapo hicho kipo kama ifuatavyo: Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu ambaye Yupo kila mahali. Mimi nina imani thabiti juu ya uongozi wa Khalifa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Ninaahidi kuwa sitampigia kura ya ndiyo mtu yeyote ambaye dhidi yake tangazo la kuwa yeye si Ahmadiyya limetolewa. Vile vile sitampigia kura ya ndiyo yule ambaye tangazo la yeye kushirikiana na wapinzani wa Jamaat limetolewa dhidi yake, na kwamba yeye ni adui wa uongozi wa Ukhalifa ndani ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya."

Ilifuata zamu ya Mirza Tahir Ahmad kula kiapo kilichowekwa kwa ajili ya makhalifa pindi wanapochaguliwa: Naapa kwa jina la Mwenyezi Mngu Aliye Hai kuwa nina imani thabiti juu ya uongozi wa Ukhalifa katika Jamaat ya Ahmadiyya. Nami nawahesabu wale wote wanaonipinga kuwa wako kwenye njia iliyopotea. Nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kuulinda Ukhalifa na kuhakikisha unadumu mpaka siku ya kiyama. Pia nitafanya kila linalowezekana kufikisha ujumbe wa dini ya kiislamu katika pembe zote za dunia.

Nitasimamia haki za watu wote, nalo litakuwa jukumu langu la kwanza bila ya kujali hali zao na mali zao. Matajiri au masikini, wanaume na wanawake. Nitafanya hivyo kwa moyo wangu wote na nguvu zangu zote, huku nikipata msaada wa jamaat. Nitafanya juhudi zote kufikisha elimu ya Kurani na hadithi za Mtume s.a.w kwa watu wote wa ulimwengu". Baada ya viapo hivi ilifuatia kipindi cha kufanya ahadi ya utii kwa Khalifa (Baiat). Kwa ufupi Baiat historia yake inaanzia kwa Mtume s.a.w. Huu ni mkataba wa biashara anaofanya mja na Mola wake. Kwamba yeye anauza nafsi yake ili apate radhi ya Mola wake. Hivyo amri yoyote atakayopewa kutoka kwake ataitii kwa jazba na ari. Hakitakuwepo kikwazo cha aina yoyote cha nafsi yake kwani imeshauzwa kwa Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa Khalifa ni mwakilishi wake Mwenyezi Mungu basi ndio maana ahadi hii inachukuliwa na Khalifa. Baiat ni utii wa moja kwa moja kwa Khalifa.

Mtu anayefanya Baiat huapa:-

"Nashuhudia ya kuwa hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu. Yu mmoja hasiye na mshirika. Na ninashuhudia kuwa Muhammad s.a.w. ni mtumishi wake na Mtume wake.

Leo mimi ninajiunga na Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya kwa mkono (jina la Khalifa wa wakati husika aliyechaguliwa). Nina imani thabiti kuwa Muhammad s.a.w. ni mjumbe wa MwenyeziMungu na ni khatamun-Nabiyyina (Muhuri wa Manabii). Nami ninakiri kuwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s wa Qadian ndiye yule yule Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa ambaye bishara ya kuja kwake ilitolewa na Mtume Muhammad s.a.w.

Ninaahidi ya kwamba nitajitahidi kutekeleza masharti kumi ya BAIAT yaliyowekwa na Masihi aliyeahidiwa a.s. Nitatanguliza dini juu ya dunia. Daima

Itaendelea Toleo lijalo, Inshaallah.

MWENYEZI MUNGU ALIVYOWAPASHA HABARI ZA GHAIBU WAAMINIO KUHUSU KHALIFA WA TANO

Kutoka Uk. 12

Imefasiriwa na Jamil Mwanga, Dar es Salaam

Katika aya Istikhlaf (Sura Al-Nur, Aya 56), waaminio wamepewa habari njema kwamba ikiwa wataendelea kubakia katika hali ya kuamini na kufanya vitendo vizuri, Allah atawajaalia Ukhalifa. Aya hii i wazi katika madai yake kwamba Khalifa huchaguliwa na Allah mwenyewe.

Waaminio hupewa nafasi ya kuonesha chaguo lao lakini hakuna shaka yoyote kwamba hukaa na kukubaliana kumchagua mtu ambaye tayari ni chaguo la Mwenyezi Mungu.

Zaidi ya hayo, Allah huwaimarisha waaminio kwa njia ya kuwapasha habari baadhi yao wakiwa wanaume, wanawake na hata watoto katika namna mbalimbali za uwazi, kuhusu chaguo lake ili kwamba baadaye waweze kuwa ni wenye kushuhudia pindi matukio yanapodhihirika. Hii huwaimarishia zaidi imani yao.

Imegundulika kwamba watu hawa wenye bahati kubwa, huieleza na kuichukulia kwa uaminifu habari hii, na huisimulia tu kwa baadhi ya ndugu au jamaa wa karibu.

Kabla ya kuchaguliwa Khalifa wa Tano, palikuwepo na mamia ya watu ambao walionyeshwa ndoto bayana juu ya matokeo ya uchaguzi huo. Baadhi ya ruya za watu hao zinaelezwa hapa.

1. Bw. Maqsoodul Haq, mtoto wa Hayati Maulana Abdul Munir Noorul Haq ameandika katika barua yake ya Agosti, 28, 2003:

"Leo ninamwita mama yangu kuthibitisha yafuatayo kama alivyonisimulia:
'takribani miaka miwili hadi mitatu kabla baba yako hajafariki (Desemba 30, 1995), alipoamka asubuhi alinieleza kwamba katika ndoto aliona chumba kikiwa na watu wa familia ya Masihi Aliyeahidiwa wakiwa wameketi katika duara. Hadhrat Khalifatul Masih III (Rehema ya Allah iwe juu yake) akawasili akiwa amebeba mikufu miwili mikononi mwake, mmoja mdogo na mwingine mkubwa. Akawaangalia watu wale na kuuweka ule mkufu mkubwa kwa Sahibzada Mirza Masroor Ahmad Sahib na ule mdogo akauweka kwa mzee mwingine mwanaume. Baada ya kusimulia ndoto yake baba yako alisema kwamba inaelekea kwamba Allah anakusudia kuwapa majukumu muhimu watu hawa wawili. Aliendelea kusema kwamba ameniambia ndoto hii kwa vile huenda asiwe hai pindi tukio hili litakapotokea.' Mama yangu alisema kwamba ingawa aliyeona ndoto hii huenda akawa alitumia maneno tofauti na haya lakini maana yake hasa ni kama ilivyotajwa hapo."

2. Bw. Ikram Ullah Cheema wa Ujerumani amemwandikia Hazoor:

"Mwaka 1997 niliona ndoto kwamba unatembelea nyumbani kwangu huko Rabwah ukiwa umevaa 'kilemba' cha Hazoor na pia mavazi uliyovaa ni kama ya 'Hazoor'. Nilikutambua kama 'Hazoor'. Nikauliza yu wapi mlinzi (bodyguard)?

Halafu nikauliza tukio hili litatimiaje? Ulijibu kwamba ni baraka za Allah alizokujaalia.

Kufumba na kufumbua nikahisi kama vile umezama katika hisia za shukrani kwa Mola wako. Nikaushika mkono wako na baada ya kufanya hivyo ukatokeza na kuanza kutembea tena. Katika ndoto ile niliambiwa kwamba jina lako ni Masroor Ahmad. Nilikuwa sijawahi kukutana nawe hapo kabla. Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba baada ya miaka kumi nilitembelea Rabwah nilikuona na kukukuta kama nilivyokuona kwenye ndoto. Katika ndoto uso wako ulikuwa na nuru ambayo sikuwahi kuiona hapo kabla."

3. Bw. Shaikh Umar Ahmad Munir, mtoto wa hayati Bw. Shaikh Noor Ahmad Munir wa Rawalpindi ameandika:

"Ninaapa kwa jina la Allah kwamba Desemba 1999 niliona ruya ifuatayo: Nilikuwa naingia msikitini huko Islamabad (Pakistan) na kumwona Bw. Ayubi ambaye ni dereva wa Hadhrat Khalifatul Masih III (Rehema ya Allah iwe juu yake) akiwa nje ya chumba kikubwa. Nikamwuliza ni kwa nini amekaa nje ilhali kila mmoja yu ndani anasali. Alisema kwamba yuko pale kwa ajili ya kufanya ulinzi kwa yule atakayechaguliwa kuwa Khalifa. Nikasema kwamba nami ningependa pia kumwona yule atakayekuwa amechaguliwa kuwa Khalifa. Baada ya kusisitiza, alinitaka niahidi kwamba sitamweleza yeyote habari hii. Nilipoingia ndani ya chumba hicho nilimwona Sahibzada Mirza Masroor Ahmad na baada ya hapo niliamka toka usingizini."

4. Bi Amatul Naseer Munir wa Mohalla Darul Nasr Pakistan Magharibi, ameandika:

"Mwaka 1999, katika mwezi ule ambao Sahibzada Mirza Qadir Sahib aliuwawa shahidi, niliona (katika ndoto) kwamba ninaingia katika chumba. Ndani yake si chumba bali ukumbi mkubwa. Nikatembea hatua chache nikiwa humo ndani na kumwona Hadhrat Khalifatul Masih IV (rehema ya Allah iwe juu yake) akiendesha darasa la Kiurdu (Urdu class) huku akiwa ameuelekeza uso wake mlangoni. Nikasikia sauti kutoka nje na niligeuka ili kuangalia kulikoni, lakini sikumwona mtu yeyote. Nilipogeuka tena kumwangalia Hazoor nikaona kwamba ametoweka na nafasi yake imechukuliwa na mtu mwingine mwenye umri wa kati (middle aged person). Nikamwangalia mtu huyo kwa karibu na kisha nikaamka. Mpendwa Hazoor, sikuwahi kumwelezea mtu yeyote ndoto hii. Niliendelea kuomba kwa unyenyekevu na kulia mbele ya Allah kutokana na uthibitisho wa mtu yule niliyemwona.
Siku moja nilifika ofisini kwa *Ameer Muqami* nikiomba kwa niaba ya Halqa Lajna wetu kuhusiana na kutumia mali yako katika *Ahmad Nagar*. Nilipoingia, nawe ukanitazama, ghafla nililowa jasho juu hadi chini, kwa sababu uso wa mtu niliouona katika ndoto ile ni wa kwako.

5. Bw. Nasir Mahmood Ahmad ameandika katika barua yake ya Mei 10, 2003:

"Miaka miwili iliyopita wakati nilipokuwa ninafanya kazi huko Kanakri, katika ndoto niliona mtu mmoja ananionesha picha kubwa ikiwa katika 'frame'. Picha hiyo ilikuwa ni ya mtu aliyevaa kilemba. Huyu ni nani? Aliuliza. Ilisikika sauti ikijibu kwamba huyu ni Khalifa mtarajiwa. Nikauliza jina lake ni nani. Na sauti ikasema, 'Mirza Masroor Ahmad.' Siku iliyofuata nilimsimulia ndoto hii Maulana Khushi Muhammad Shakir, Mbashiri wa Guinea Kanakri. Aliniambia nijizuie kueneza habari hii mpaka tukio hilo litimie. Baada ya kufariki kwa Hadhrat Khalifatul Masih IV (Rehema ya Allah iwe juu yake), lakini kabla ya uchaguzi nilimsimulia mama yangu kuhusu ndoto hii.

6. Bi. Amatul Musawwir wa Darul Uloom Sharqi, Rabwah ameandika katika barua yake ya Januari 21, 2004:

"Ninapenda kusimulia ndoto yangu niliyoota Aprili 23, 2002. Niliona kwamba ninasikiliza

SALAMU ZA AMIR SAHIB

Kutoka Uk. 12

Ndugu zangu wapendwa, mabibi na mabwana Assalaam Alaikum warahmatullah wabarakaatuh.

Awali ya yote hatuna budi kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia kuiona siku hii muhimu ya leo, ambapo tunaadhimisha miaka mia moja (100) ya Ukhalifa wa Kiahmadiyya.

Napenda niwakaribisheni nyote katika mkutano huu adhimu na ninamuomba Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kuwa wanyenyekevu, watulivu na wenye kumkumbuka sana Mwenyezi Mungu, ili tuweze kunufaika na siku hii ya leo.

Ndugu zangu wapendwa, siku hii ni muhimu kutokana na kutimia kwa ahadi ya Mwenyezi Mungu Aliyoitoa katika Qur'an Tukufu ya kwamba ***"Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu hawatanishirikisha na chochote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri"*** (Qur'an Tukufu 24:56)

Ahadi hii ilitimia kwa muda mfupi wa takriban miaka 30 baada ya kufariki kwa Mtume Muhammad (s.a.w) na ikatimia tena baada ya takriban karne 14 kupita.

Sherehe za leo ambazo zitaelezwa kwa kirefu katika hotuba zitakazofuata hapo baadaye, zinahusu Ukhalifa wa awamu ya pili baada ya Mtume (s.a.w). Ukhalifa huu ambao tunasherehekea hivi leo, ulianza tarehe 27 Mei 1908 kufuatia kufariki kwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s) ambaye ni Masihi Aliyeahidiwa na Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya.

Hivyo sherehe hii ya leo ni ya shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kutimiza ahadi yake ya kuteua viongozi - yaani Makhalifa ndani ya Uislam - hususan katika Silsila ya Ahmadiyya, kwa mfululizo katika kipindi cha miaka mia moja (100), Alhamdulillah.
Ndugu zangu wapendwa, kimsingi Ukhalifa ni uongozi unaowekwa na Mwenyezi Mungu.

Katika Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya hadi tunapofanya sherehe hizi za karne au miaka 100 ya Ukhalifa, tunaye Khalifa wa tano ambaye ni Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (Mwenyezi Mungu Amsaidie kwa msaada wake adhimu).

Makhalifa, kama viongozi waliowekwa na Mwenyezi Mungu, husimamia na kustawisha sheria za Mwenyezi Mungu - yaani mafundisho halisi ya dini ya Kiislam, ambayo hayana ubaguzi wa kijinsia, kidini, kikabila, rangi n.k.

Kwa neno zima makhalifa husimamia harakati za kuwarudisha watu kwa Mwenyezi Mungu Mmoja - yaani 'Allah' na hivyo kujenga mazingira murua ya umoja, utii, mapenzi, ushirikiano n.k. baina ya watu.

Hivi leo ndugu zangu wapendwa, sifa hizo njema zinapatikana kwa wingi mno miongoni mwa Waahmadiyya, chini ya uongozi wa Khalifa.
Ukhalifa umetuwezesha sisi Waahmadiyya wa mataifa mbalimbali kujuana na kupendana. Pia Ukhalifa umetuwezesha kwa kiasi kikubwa kuwa Raia wema (yaani wafuataji wa sheria) katika nchi mbalimbali duniani.
Aidha Ukhalifa umetuwezesha kuwa na mfumo mzuri wa utawala ndani ya Jumuiyya yetu ambao unamtambua kila Ahmadiyya na hivyo kumjengea mazingira yatakayomwezesha kufanya bidii katika ibada kwa amani bila bughudha yoyote.
Halikadhalika Ukhalifa, kupitia mipango mbalimbali umetupatia fursa ya kuchota elimu ya dini katika bahari kubwa ya elimu aliyopewa Masihi Aliyeahidiwa (a.s).

Ndugu zangu wapendwa haya si madai matupu bali ulimwengu mzima ni shahidi wa haya yote.

Pamoja na hayo yote ni muhimu tukumbuke kuwa Khalifa hayupo tu kwa ajili yetu sisi ambao tumeshajiunga na Jumuiyya hii tukufu, bali anawajali pia binaadamu wote kwa jumla, ambao ni viumbe vya Mwenyezi Mungu Ambaye anamwakilisha katika uongozi hapa duniani. Msemo maarufu katika Jumuiyya yetu wa ***"Love for all hatred for none" yaani "Mapenzi kwa wote chuki si kwa yeyote"*** unaashiria jambo hili.
Ndugu zangu wapendwa, kwa kuangalia hali halisi iliyopo duniani hivi sasa, ambapo ubinafsi, udhalimu, ufisadi ni magonjwa yanayozitesa jamii mbalimbali duniani, ni dhahiri kuwa Ukhalifa ni uongozi ambao unahitajika sana kwa ajili ya ustawi wa kimwili na kiroho duniani.

Uongozi huu unahitajika ili kuwafanya wanadamu wanufaike na neema mbalimbali za Mwenyezi Mungu.

Hivi leo kwa masikitiko makubwa tunaona ya kwamba kuwa na ardhi nzuri, madini mengi, mafuta n.k. si lazima kuwa chanzo cha neema kwa jamii husika bali aghalabu huwa ni chanzo cha vita na mateso mbalimbali ndani ya jamii hizo kwa kuchochewa na wenye nguvu za kijeshi na kiuchumi.

Uhasama unaozalika kutokana na hali hiyo hauwapi utulivu wanyonge (masikini) wala wenye nguvu (matajiri). Hivi leo hofu ya usalama imetanda duniani kote.
Tukumbuke ya kwamba ipo ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kuleta amani baada ya hofu (24:56), lakini ahadi hiyo imeambatana na Ukhalifa.
Hivyo wakati huu tunapoadhimisha miaka 100 ya Ukhalifa ni vema tukumbushane wale wote tuliokubali Ukhalifa ya kwamba ni muhimu tusimame imara katika kuamini na kutenda vitendo vizuri (24:56) hayo ni masharti ya kuendelea kunufaika na Ukhalifa. Wakati huo huo hatuna budi tuzidishe juhudi za kuueneza Ukhalifa kwa wenzetu ili tuwe wengi wenye kufuata uongozi huu wa kimbingu, ili hatimaye watu wema wazidi katika sura ya ardhi na kuifanya ardhi pawe mahali pema pa kuishi na kutafuta maisha ya akhera.
Ninamuomba Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kusherehekea siku hii ya leo kwa amani na usalama na tupate kheri nyingi za Ukhalifa. Amin.
Akhsanteni kwa kunisikiliza.

Wassalaam Alaikum
Alli Saidi Mosse
Amir Jamaat Ahmadiyya - Tanzania

First Muslim Newspaper in Kiswahili Language started in 1936

Mafundisho ya Mtume s.a.w.

Mtume s.a.w. alisema: ... Aliyekufa ilhali hakufanya baiati ya Imam wa zama zake amekufa kifo cha kijinga. (Muslim).

MAPENZI YA MUNGU

Toleo Maalum la Karne ya Ukhalifa, Mei 2008

TOLEO MAALUM LA KARNE YA UKHALIFA 1908 - 2008

MWENYEZI MUNGU ALIVYOWAPASHA HABARI ZA GHAIBU WAAMINIO KUHUSU KHALIFA WA TANO

Imefasiriwa na Jamil Mwanga, Dar es Salaam

Katika aya Istikhlaf (Sura Al-Nur, Aya 56), waaminio wamepewa habari njema kwamba ikiwa wataendelea kubakia katika hali ya kuamini na kufanya vitendo vizuri, Allah atawajaalia Ukhalifa. Aya hii i wazi katika madai yake kwamba Khalifa huchaguliwa na Allah mwenyewe.

Waaminio hupewa nafasi ya kuonesha chaguo lao lakini hakuna shaka yoyote kwamba hukaa na kukubaliana kumchagua mtu ambaye tayari ni chaguo la Mwenyezi Mungu.

Zaidi ya hayo, Allah huwaimarisha waaminio kwa njia ya kuwapasha habari baadhi yao wakiwa wanaume, wanawake na hata watoto katika namna mbalimbali za uwazi, kuhusu chaguo lake ili kwamba baadaye waweze kuwa ni wenye kushuhudia pindi matukio yanapodhihirika. Hii huwaimarishia zaidi imani yao.

Imegundulika kwamba watu hawa wenye bahati kubwa, huieleza na kuichukulia kwa uaminifu habari hii, na huisimulia tu kwa baadhi ya ndugu au jamaa wa karibu.

Kabla ya kuchaguliwa Khalifa wa Tano, palikuwepo na mamia ya watu ambao walionyeshwa ndoto bayana juu ya matokeo ya uchaguzi huo. Baadhi ya ruya za watu hao zinaelezwa hapa.

1. Bw. Maqsoodul Haq, mtoto wa Hayati Maulana Abdul Munir Noorul Haq ameandika katika barua yake ya Agosti, 28, 2003:

"Leo ninamwita mama yangu kuthibitisha yafuatayo kama alivyonisimulia:
'takribani miaka miwili hadi mitatu kabla baba yako hajafariki (Desemba 30, 1995), alipoamka asubuhi alinieleza kwamba katika ndoto aliona chumba kikiwa na watu wa familia ya Masihi Aliyeahidiwa wakiwa wameketi katika duara. Hadhrat Khalifatul Masih III (Rehema ya Allah iwe juu yake) akawasili akiwa amebeba mikufu miwili mikononi mwake, mmoja mdogo na mwingine mkubwa. Akawaangalia watu wale na kuuweka ule mkufu mkubwa kwa Sahibzada Mirza Masroor Ahmad Sahib na ule mdogo akauweka kwa mzee mwingine mwanaume. Baada ya kusimulia ndoto yake baba yako alisema kwamba inaelekea kwamba Allah anakusudia kuwapa majukumu muhimu watu hawa wawili. Aliendelea kusema kwamba ameniambia ndoto hii kwa vile huenda asiwe hai pindi tukio hili litakapotokea.' Mama yangu alisema kwamba ingawa aliyeona ndoto hii huenda akawa alitumia maneno tofauti na haya lakini maana yake hasa ni kama ilivyotajwa hapo."

2. Bw. Ikram Ullah Cheema wa Ujerumani amemwandikia Hazoor:

"Mwaka 1997 niliona ndoto kwamba unatembelea nyumbani kwangu huko Rabwah ukiwa umevaa 'kilemba' cha Hazoor na pia mavazi uliyovaa ni kama ya 'Hazoor'. Nilikutambua kama 'Hazoor'. Nikauliza yu wapi mlinzi (bodyguard)?

Halafu nikauliza tukio hili litatimiaje? Ulijibu kwamba ni baraka za Allah alizokujaalia.

Kufumba na kufumbua nikahisi kama vile umezama katika hisia za shukrani kwa Mola wako. Nikaushika mkono wako na baada ya kufanya hivyo ukatokeza na kuanza kutembea tena. Katika ndoto ile niliambiwa kwamba jina lako ni Masroor Ahmad. Nilikuwa sijawahi kukutana nawe hapo kabla. Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba baada ya miaka kumi nilitembelea Rabwah nilikuona na kukukuta kama nilivyokuona kwenye ndoto. Katika ndoto uso wako ulikuwa na nuru ambayo sikuwahi kuiona hapo kabla."

3. Bw. Shaikh Umar Ahmad Munir, mtoto wa hayati Bw. Shaikh Noor Ahmad Munir wa Rawalpindi ameandika:

"Ninaapa kwa jina la Allah kwamba Desemba 1999 niliona ruya ifuatayo: Nilikuwa naingia msikitini huko Islamabad (Pakistan) na kumwona Bw. Ayubi ambaye ni dereva wa Hadhrat Khalifatul Masih III (Rehema ya Allah iwe juu yake) akiwa nje ya chumba kikubwa. Nikamwuliza ni kwa nini amekaa nje ilhali kila mmoja yu ndani anasali. Alisema kwamba yuko pale kwa ajili ya kufanya ulinzi



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih V a.t.b.a

kwa yule atakayechaguliwa kuwa Khalifa. Nikasema kwamba nami ningependa pia kumwona yule atakayekuwa amechaguliwa kuwa Khalifa. Baada ya kusisitiza, alinitaka niahidi kwamba sitamweleza yeyote habari hii. Nilipoingia ndani ya chumba hicho nilimwona Sahibzada Mirza Masroor Ahmad na baada ya hapo niliamka toka usingizini."

4. Bi Amatul Naseer Munir wa Mohalla Darul Nasr Pakistan Magharibi, ameandika:

"Mwaka 1999, katika mwezi ule ambao Sahibzada Mirza Qadir Sahib aliuwawa shahidi, niliona (katika ndoto) kwamba ninaingia katika chumba. Ndani yake si chumba bali ukumbi mkubwa. Nikatembea hatua chache nikiwa humo ndani na kumwona Hadhrat Khalifatul Masih IV (rehema ya Allah iwe juu yake) akiendesha darasa la Kiurdu (Urdu class) huku akiwa ameuelekeza uso wake mlangoni. Nikasikia sauti kutoka nje na niligeuka ili kuangalia kulikoni, lakini sikumwona mtu yeyote. Nilipogeuka tena kumwangalia Hazoor nikaona kwamba ametoweka na nafasi yake imechukuliwa na mtu mwingine mwenye umri wa kati (middle aged person). Nikamwangalia mtu huyo kwa karibu na kisha nikaamka. Mpendwa Hazoor, sikuwahi kumwelezea mtu yeyote ndoto hii. Niliendelea kuomba kwa unyenyekevu na kulia mbele ya Allah kutokana na uthibitisho wa mtu yule niliyemwona.
Siku moja nilifika ofisini kwa **Ameer Muqami** nikiomba kwa niaba ya Halqa Lajna wetu kuhusiana na kutumia mali yako katika **Ahmad Nagar**. Nilipoingia, nawe ukanitazama, ghafla nililowa jasho juu hadi chini, kwa sababu uso wa mtu niliouona katika ndoto ile ni wa kwako.

5. Bw. Nasir Mahmood Ahmad ameandika katika barua yake ya Mei 10, 2003:

"Miaka miwili iliyopita wakati nilipokuwa ninafanya kazi huko Kanakri, katika ndoto niliona mtu mmoja ananionesha picha kubwa ikiwa katika 'frame'. Picha hiyo ilikuwa ni ya mtu aliyevaa kilemba. Huyu ni nani? Aliuliza. Ilisikika sauti ikijibu kwamba huyu ni Khalifa mtarajiwa. Nikauliza jina lake ni nani. Na sauti ikasema, 'Mirza Masroor Ahmad.' Siku iliyofuata nilimsimulia ndoto hii Maulana Khushi Muhammad Shakir, Mbashiri wa Guinea Kanakri. Aliniambia nijizuie kueneza habari hii mpaka tukio hilo litimie. Baada ya kufariki kwa Hadhrat Khalifatul Masih IV (Rehema ya Allah iwe juu yake), lakini kabla

Endelea Uk. 11

SALAMU ZA AMIR SAHIB KATIKA KUADHIMISHA KARNE YA UKHALIFA



Bw. Alli Saidi Mosse - Amir Jamaat Ahmadiyya Tanzania.

ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu hawatanishirikisha na chochote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri" (Qur'an Tukufu 24:56)

Ahadi hii ilitimia kwa muda mfupi wa takriban miaka 30 baada ya kufariki kwa Mtume Muhammad (s.a.w) na ikatimia tena baada ya takriban karne 14 kupita.

Endelea uk. 11

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Alli Saidi Mosse - Amir Jamaat.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Abdulrahim Nasibu.
3. Jamil Mwanga.

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Gazeti hili hutolewa na Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania na hupigwa chapa na Ahmadiyya Printing Press, S.L.P. 376 Dar es Salaam. Limesajiliwa na Mkuu wa Posta